# Vodacom Tanzania PLC
## Taarifa ya Mwaka

kwa mwaka ulioishia tarehe
31 Machi 2019



Yajayo yanafurahisha
**Uko tayari?**

vodacom

## Yaliyomo


**Maelezo ya jumla**
1 Sisi ni nani
2 Ufanisi wetu
3 Thamani tunayoijenga

**Biashara yetu**
6 Vodacom Tanzania kwa ufupi
7 Bidhaa na Huduma zetu
8 Taarifa ya Mwenyekiti
10 Ripoti ya Mkurugenzi Mtendaji

**Mazingira ya Biashara**
12 Uhusaniano na wadau

**Utendaji wetu**
14 Ufanisi wetu kifedha

**Mfumo wa kiutawala**
16 Viongozi wetu
18 Tamko la utekelezaji
20 Shughuli za uongozi wa kampuni
22 Kamati ya Uteuzi na Ujira

**Taarifa za ziada**
24 Taarifa ya Mkutano Mkuu
29 Fomu ya Mwakilishi
31 Taarifa kuhusu umiliki
31 Taarifa za Kampuni


## Maelezo ya msingi

Tafadhali zingatia kuwa hii ni tafsiri ya taarifa ya mwaka kwa ufupi. Taarifa kamili ya mwaka imetolewa kwa lugha ya kiingereza. Iwapo kutatokea mkanganyiko wa tafsiri, taarifa ya kiingereza itatumika.

# Taarifa ya mwaka ya Vodacom Tanzania PLC 2019

Hii ni taarifa ya tatu ya mwaka ya Vodacom Tanzania, na ya pili tangu kuorodheshwa kwenye soko la hisa la Dar es Salaam tarehe 15 Agosti 2017.

Taarifa hii inatoa maelezo ya jumla ya biashara yetu, mfumo wetu wa biashara, mazingira ya utendaji, kupitia mikakati yetu ya utendaji na tathmini ya mfumo wa utawala kwa mwaka wa fedha ulioanzia Aprili 2018 na kuishia Machi 31, 2019. Utaratibu wetu wa kutoa taarifa ya mwaka umekuwa ukiongozwa na kanuni na masharti ya Viwango vya Kimataifa vya Taarifa za Fedha (IFRS), Kanuni za Soko la Hisa la Dar es Salaam, 2016, Mfumo wa Kimataifa wa IIRC na matakwa ya Sheria ya Makampuni, 2002. Mkaguzi huru PricewaterhouseCoopers ('PwC') amethibitishia taarifa yetu ya fedha ya mwaka na ametoa hati safi (uk 63 – 65).

Bodi imeshiriki kikamilifu katika uandaaji na uwasilishaji wa taarifa hii. Bodi imeridhika kuwa taarifa hii inaelezea masuala yote muhimu na inawasilisha maelezo yaliyo na ulinganifu kuhusu utendaji wa kundi la makampuni ya Vodacom kwa kipindi husika, pamoja na mtazamo sahihi wa mkakati wetu wa kujituma. Wakurugenzi wanaamini kuwa kuchapisha maudhui ya mikakati ya Vodacom hakutaleta athari yoyote katika medani za ushindani wa kibiashara. Bodi ilipitisha ripoti hii ya mwaka ya kampuni pamoja na ripoti za hesabu za Vodacom Tanzania mnamo tarehe 17 Julai 2019.

Imesainiwa kwa niaba ya Bodi:

**Ali A Mufuruki**
Mwenyekiti wa Bodi

**Hisham Hendi**
Mkurugenzi Mtendaji

# Sisi ni nani

Vodacom Tanzania PLC ('Vodacom Tanzania') ni kampuni inayoongoza Tanzania kwa kutoa huduma za mawasiliano ya simu na huduma za miamala ya fedha kwa njia ya simu, ikiwa na watumiaji huku zaidi ya asilimia 90 ya watumiaji hao wakipata huduma za simu za kiganjani, mtandao mpana wa data wenye kasi kubwa na mtandao mkubwa zaidi Tanzania wa miamala ya malipo kwa njia za simu. Tunatoa huduma mbalimbali za mawasiliano kwa watumiaji na makampuni – ikiwa ni pamoja na huduma za kuzungumza katika simu, data na ujumbe mfupi, video, cloud na host, programu za simu na huduma za kifedha – kwa zaidi ya wateja milioni 14.1.

**Vodacom Tanzania iliorodheshwa kwenye soko la hisa la Dar es Salaam mnamo Agosti 15, 2017. Mmiliki mkubwa wa Vodacom Tanzania na kampuni zake tanzu (yaani 'Kundi la Kampuni za Vodacom') ni Vodacom Group Limited, kampuni iliyosajiliwa Afrika Kusini ambayo nayo inamilikiwa na Vodafone Group PLC ya Uingereza.**

## Mikakati yetu

| Azma Yetu | Dira yetu | Utekelezaji | Mihimili Yetu ya Msingi |
| --- | --- | --- | --- |
| Kwanini tupo | Tunaelekea wapi | Tunataka kufanya vipi | Tunapaswa Kufanya Nini |
| Tunawaunganisha watu ili waishi maisha yaliyo bora zaidi leo na siku zijazo | Kuwa kinara wa makampuni yanayotoa huduma za kidigitali inayowezesha maisha ya kidigitali kwa jamii iliyounganishwa kidigitali. | Kasi, wepesi, kuaminiwa katika jamii iliyounganishwa kidigitali. | |




1. Ookla speed test report as at 31 March 2019

# Ufanisi wetu

## Muhtasari wa utendaji

### Mapato ya huduma yameongezeka

5.4% (asilimia 7.3* bila badiliko la MTR) kufikia **Sh bilioni 1 018.9**, ikiongozwa na ongezeko kubwa katika mapato ya M-Pesa, huduma za data na ujumbe.

Tuliongeza wateja milioni 1.2 katika mwaka huo hadi kufika **milioni 14.1m,** ongezeko la 9.6%

### EBITDA imeongezeka

8.1% kufikia **Sh bilioni 287.9** kukiwa na ongezeko dogo la alama 0.9 hadi kufika asilimia 28.1 zilizofikiwa kupitia ongezeko kubwa la mapato ya huduma ikisaidiwa na programu yetu ya kudhibiti gharama.

### Tulifanya uwekezaji mkubwa wa

Sh bilioni171.4, ili kuongeza wigo wa huduma zetu za 4G katika miji mikubwa na kuongeza ubora wa mtandao wetu.

### Faida halisi ilieongezeka kwa

33.8%[1] hadi **Sh bilioni 90.2** kimsingi kutokana na ongezeko zuri la mapato ya huduma ikisaidiwa na programu yetu ya 'Fit for Growth'.

### Mzunguko huru wa fedha uliorekebishwa uliongezeka

84.5%[2] hadi **Sh bilioni 114.9** kimsingi kutokana na kuongezeka kwa ufanisi wa biashara na vilevile usimamizi wetu imara wa mtaji wa kuendesha biashara.

### Muhtasari wa taarifa ya fedha

| Taarifa za pamoja, Sh milion | Mwaka ulioishia Machi 31<br>2019<br>IFRS 15 | <br>2019<br>IAS 18# | <br>2018<br>IAS 18 | % ya mabadiliko mwaka hadi mwaka 17/18 |
|---|---|---|---|---|
| Mapato ya huduma | **1016 237** | **1 018 910** | 966 275 | 5.4 |
| Jumla ya mapato | **1024 587** | **1 023 763** | 977 994 | 4.7 |
| Mapato kabla ya riba, kodi na uchakavu (EBITDA) | **288 656** | **287 879** | 266 370 | 8.1 |
| Mapato kabla ya riba na kodi (EBIT) | **115 682** | **114 905** | 95 509 | 20.3 |
| Faida ya uendeshaji | **115 333** | **114 556** | 88 901 | 28.9 |
| Faida halisi baada ya kodi | **90 761** | **90 217** | 170 240 | (47.0) |
| Mzunguko huru wa fedha za uendeshaji | **142 151** | **142 151** | 89 811 | 58.3 |
| Mzunguko huru wa fedha | **114 919** | **114 919** | (42 245) | >200 |
| Matumizi ya mtaji | **171 432** | **171 432** | 159 705 | 7.3 |
| Salio la fedha taslimu | **390 821** | **390 821** | 434 091 | (10.0) |
| Mapato kwa kila hisa (shilingi) | **40.52** | **40.28** | 83.81 | (51.9) |
| Kiwango cha mgawanyo (%) | **70.4** | **70.4** | 69.0 | 1.4ppts |
| Kiwango cha EBIDTA (%) | **28.2** | **28.1** | 27.2 | 0.9ppt |
| Kiwango cha mapato kabla ya riba na kodi (EBIT) (%) | **11.3** | **11.2** | 9.8 | 1.4ppt |
| Kiwango cha faida ya uendeshaji (%) | **11.3** | **11.2** | 9.1 | 2.1ppt |
| Kiwango cha kodi kinachofaa (%) | **32.7** | **32.7** | 21.3 | 11.4ppt |
| Kiwango cha faida halisi (%) | **8.9** | **8.8** | 17.4 | (8.6)ppts |
| Salio la fedha taslimu/EBITDA (times) | **1.4** | **1.4** | 1.6 | (0.2)ppts |
| Matumizi ya mtaji (%) | **16.7** | **16.7** | 16.3 | 0.4ppts |

Kufuatia uamuzi wa kutumia IFRS 15, mapato kutokana na Mikataba na wateja tarehe 1 Aprili 2018, matokeo ya Kampuni kwa miezi kumi na miwili iliyoishia tarehe 31 Machi 2019 yamezingatia utaratibu wa IFRS 15, wakati matokeo kwa miezi kumi na miwili iliyoishia tarehe 31 Machi 2018 yaliwasilishwa (kama ilivyoripotiwa awali) katika kiwango cha IAS 18. Ulinganishi kati ya viwango viwili vya ripoti huana maana sana na ili kuhakikisha taarifa zinatolewa kwa usahihi wakati wa kipindi cha mpito kwenda katika IFRS 15, viwango fulani vya kifedha kwa miezi kumi na miwili iliyoishia tarehe 31 Machi 2019 imeelezwa kote katika kiwango cha IFRS 15 na IAS 18 na maoni yetu kufafanua ufanisi wetu kiuendeshaji katika mapitio ya uendeshaji na fedha umetolewa kimsingi katika kiwango cha IAS 18. Athari za kutumia kiwango hiki kipya si muhimu kwa Kampuni, na hivyo ufafanuzi na maoni zaidi kuhusu matokeo yatazingatia IAS 18 mwaka wa fedha. Kiwango cha hesabu kilichotumika kinaonekana wazi katika vichwa vya safu husika katika taarifa zinazotolewa.

1. Ukiondoa faida ya mwaka uliopita kutokana na mauzo ya hisa zisizo na riba katika Helios Towers na malipo ya hisa.
2. Imerekebishwa kwa riba ya Sh bilioni 104.6 katika mkopo kutoka kwa Vodacom Group uliolipwa na Vodacom kutokana na mzunguko wa fedha zilizozalishwa ndani.

# Thamani tunayojenga

## Kwa wanahisa wetu

Tumewalipa wanahisa wetu Sh bilioni 38.8 (2018: Sh bilioni 28.5) kama gawio

## Kwa wateja wetu

### Tumepanua mtandao wetu

**Tumeongeza minara 322 yenye huduma ya 4G, 197 yenye huduma ya 3G na 73 yenye huduma ya 2G**

| Huduma ya 4G | Huduma ya 3G | Huduma ya 2G |
|---|---|---|
| **23%** ya idadi ya watu | **52%** ya idadi ya watu | **90%** ya idadi ya watu |

Tunaongoza kwenye tasnia kwa kupata mrejesho chanya wa kiwango cha ubora wa huduma zetu (NPS) – kigezo muhimu cha kupima jinsi wateja wanavyoridhishwa na huduma zetu;tunaongoza kwa alama 12.

Mtandao unaotoa huduma ya data wenye kasi zaidi nchini

**Tuna wateja amilifu zaidi ya**

milioni 14.1

ambapo zaidi ya wateja **milioni 7.0** wanatumia huduma zetu za kifedha za M-Pesa.

## Kwa wafanyakazi wetu

Tuna jumla ya wafanyakazi wa kudumu 548

**Tumewekeza Shilingi**

bilioni 59

kama ujira, mafunzo, na kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma

Tumetoa mafunzo ya uongozi na utawala kwa mameneja wa kada za kati na juu

## Mchango wetu katika jamii

Tumelipa sh bilioni 350 kwa watoa huduma wa ndani na wabia takribani 300 nchini **Tanzania**.

Vodacom Tanzania Foundation, Vodafone Foundation na wabia wao kwa pamoja wamewezesha kutoa fedha **zaidi ya**

Shilingi bilioni 11

katika kuhamasisha masuala ya kijamii nchini Tanzania kuanzia mwaka 2014.

**Kiasi cha**

Sh trilioni 1.1

(2019: TZS0.4 trillion) kimelipwa kwenye mfuko wa serikali kupitia kodi, gharama za masafa na tozo kwa Mamlaka ya usimamizi wa huduma katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Vodacom pamoja na mtandao wake wa huduma ya kifedha inakadiriwa kutengeneza nafasi za ajira zaidi ya

127 000

# **Miaka 18** ya kuunganisha na kuiwezesha jamii

**2000** kuanza kutoa huduma (za mawasiliano ya sauti, ujumbe mfupi na faksi)

**2002** Wateja laki 3

**2006** Vodacom Tanzania Foundation ilizinduliwa

**2007** huduma ya data ya (2G; 3G na WiMax) zilianza kutolewa

**2008** huduma za data zilizinduliwa na kuanza kutolewa mikoani na kuzinduliwa kwa huduma ya M-Pesa

**2016** huduma ya data ya 4G ilizinduliwa

**2017** Kampuni ya Kimataifa Inayomilikiwa na Wananchi: Kampuni ya kwanza ya simu kuorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam.


**2019** Tunatoa huduma kwa wateja zaidi ya milioni 14.1 nchini



| 2008 | 2010 | 2012 | 2014 | 2019 |
|---|---|---|---|---|
| Huduma ya M-Pesa ilizinduliwa. | 2010 Huduma ya malipo kutoka kwa mteja kwenda kwa mfanyabiashara na kutoka kwa mfanyabiashara kwenda kwa mteja ilizinduliwa. Huduma ya biashara ya kukusanya na kulipa fedha za serikali . | Mabenki na huduma za umma ziliunganishwa katika huduma za M-Pesa | 2014 Huduma za Kuweka Akiba na Kutoa Mikopo, Malipo ya Wafanyabiashara na Kutuma Fedha Kimataifa zilianzishwa. | Zaidi ya wateja milioni 9.0 wanatumia huduma yetu ya M-Pesa ndani ya siku 90 |

# **Miaka 11** ya kutoa huduma za miamala ya kifedha kwa watu wengi nchini Tanzania







**Mgawanyo wa umiliki wa soko[1]**



| | |
|---|---|
| Vodacom | 32% |
| Mshindani A | 28% |
| Mshindani B | 26% |
| Mshindani C | 8% |
| Wengineo | 6% |

**Mgawanyo wa umiliki wa soko la huduma za kifedha[1]**



| | |
|---|---|
| M-Pesa | 40% |
| Mshindani A | 33% |
| Mshindani B | 18% |
| Mshindani C | 6% |
| Wengineo | 3% |

1. Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania ('TCRA') takwimu ya robo mwaka iliyoishia tarehe 31 Machi 2019.

# Vodacom Tanzania kwa ufupi


## Inahudumia watu

2G inahudumia watu
90%


3G inahudumia watu
52%


4G inahudumia watu
23%

## Mtandoa




# Maelezo ya ongezeko la thamani



# Bidhaa na huduma zetu

Tuna **wateja amilifu** zaidi ya **milioni 14.1** wanaotumia bidhaa na huduma zetu za aina mbalimbali. Tumeendelea kuwa kinara katika soko kwa kuanzisha bidhaa na huduma mbalimbali mpya nchini.

## M-Pesa

M-Pesa inaendelea kuongoza katika kutoa bidhaa na huduma za kibunifuna kufanya maisha ya wateja wake kuwa rahisi na bora, huku miamala yenye thamani ya karibu **Sh trilioni 4.1** ikifanyika kupitia M-Pesa kila mwezi.

**Fedha zinazoingizwa na kutolewa:**

Zaidi ya wateja milioni 7 wa M-Pesa waliingiza and kutoa pesa katika akaunti zao za M-Pesa kupitia mawakala zaidi ya **10 6000** nchini kote na kwa gharama nafuu.

**Uhamishaji fedha kutoka kwa mtu kwenda mtu mwingine:**

Hii huwawezesha wateja wa Vodacom Tanzania kutuma fedha kwa wateja wa mitandao mingine ya simu.

**Lipa kwa M-Pesa:**

Mfumo wetu wa M-Pesa huwawezesha wafanyabiashara kupokea malipo kwa ajili ya bidhaa na huduma zilizouzwa kwa wateja wa Vodacom na wale wa washindani wetu. Katika mwaka huu, hii imekuwa njia nyepesi zaidi ya malipo kielektroniki ambayo ni chaguo kwa Watanzania kupitia jukwaa letu la zaidi ya wafanyabiashara **11 000**, wanaozidi idadi ya vituo mbadala vya malipo ya kielektroniki nchini kote.

**M-Pawa:**

Bidhaa yetu ya ki mapinduzi ya kuweka akiba na kupata mkopo, M-Pawa, inawawezesha wateja kuweka akiba kwenye akaunti ya akiba, na kutoa fedha za mkopo kwa malipo kidogo yanayolipwa kwa M-pesa. Katika nchi ambayo watu wengi hawawezi kupata huduma rasmi za kibenki, M-Pawa inaendeleza juhudi muhimu za kuwajumuisha watu katika masuala ya fedha.

**Uhamishaji wa Fedha Kimataifa:**

Wateja wa M-Pesa wanaweza kutuma fedha kwenda Kenya kwa ada kidogo kupitia akaunti zao za M-Pesa.

**Huduma za Kibiashara:**

M-Pesa inaziwezesha biashara kutuma fedha kwenye biashara nyingine (B2B) na watumiaji (akaunti za kulipia) kwa huduma kama vile malipo ya mshahara, na kwa biashara kupokea fedha kupitia M-Pesa kutoka kwa wateja wao (akaunti za makusanyo) kwa huduma kama vile kulipia bili.

## Bidhaa na huduma za walaji

**Bando za sauti, data na ujumbe mfupi wa maneno**

Zinatolewa kwa bei mbalimbali.

**Huduma zilizoongezwa thamani**

Uwanda mpana wa huduma zinazolenga makundi yote katika soko, ikiwa ni pamoja na: M-Pesa, simu, lango la runinga, huduma za televisheni kupitia iflix, programu za muziki na huduma yetu ya kutumia facebook bure bila makato.

**Huduma kwa wateja**

Madawati madogo ya huduma kwa wateja; dawati mahsusi kwa ajili ya wateja wenye thamani kubwa; programu ya kudokeza kidigitali (taarifa baada ya kupiga simu, salio halitoshi, kuisha kwa bando na kuisha muda wake).

## Vifaa

Simu za kiganjani, tableti, na modemu za broadband.

Mnamo Machi 2019 tulikuwa na zaidi ya simu janja milioni 3 zinazotumika katika mtandao wetu, ikiwa ni ongezeko la **asilimia 32.6** mwaka hadi mwaka, zinazowakilisha ongezeko la pointi 0.8 hadi **30.3** la matumizi ya vifaa janja.

## Biashara

Tunatoa huduma mbalimbali zinazohamishika na zisizohamishika kwa ajili ya biashara zinazokua, ndogo na za kati, na kundi la wenye ofisi ndogo – ofisi ya nyumbani (SoHo). Huduma hizi ni pamoja na:

**Uunganishaji**

pasi waya, waya usiohamishika; VPN; huduma ya sauti na data

**Tumemudu**

Intaneti ya vitu; APN ya shirika

**Utunzaji wa usalama wa data mitandaoni**

# Taarifa ya Mwenyekiti

Ali A. Mufuruki


**Huu umekuwa mwaka mwingine wa utendaji thabiti kwa Vodacom Tanzania PLC, kukiwa na matokeo thabiti yaliyowasilishwa katika kila moja ya nguzo za kimkakati za Kampuni hii.**



Imekuwa inafurahisha hasa kuona uongezeko katika umiliki wa soko na idadi ya wateja katika huduma zote za M-Pesa na data, kukiwa na ongezeko la 9.6% ya jumla ya wateja wetu, kufikia zaidi ya wateja milioni 14.1. Mapato ya M-Pesa yaliongezeka kwa 14.5% mwaka huu hadi kufikia Shilingi bilioni 333.5 wakati mapato ya huduma ya data yameongezeka kwa kiasi cha kuridhisha kwa 17.9% hadi Sh bilioni 167.0. Pamoja na ongezeko katika mapato ya ujumbe mfupi, kuendelea kwa mnyumbuko katika mapato ya sauti na utendaji thabiti katika programu ya Kampuni ya kupunguza gharama kumechangia katika ongezeko la 33.8% katika faida halisi, kufikia Sh bilioni 90.2. Ongezeko kubwa katika idadi ya watumiaji wa data hadi kufikia 34.2%, linaakisi mchango wa Kampuni hivi karibuni kuzindua mtandao wake wa 4G na mahitaji makubwa ya huduma zake za data. Idadi ya watumiaji wa huduma ya data ya 4G iliongezeka kwa kiasi cha kuridhisha cha asilimia 112.0, ikichangia katika idadi ya jumla ya ongezeko la watumiaji kwa 43.9%. Kutokana na idadi ndogo ya watumiaji wa intaneti na simu janja nchini Tanzania, ongezeko hili la awali linaonyesha kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kuendelea kuongezeka zaidi.


Ufanisi mzuri mwaka huu ulifanikiwa kutokana na kuwa na uendeshaji thabiti, kukiwa na mwendelezo wa shinikizo katika matumizi ya wateja, mazingira ya udhibiti yenye changamoto, na soko lenye ushindani mkubwa. Kwa upande wa udhibiti na sera, Kampuni iliathiriwa na kuendelea kushuka kwa viwango vya uunganishaji wa simu, kuanzishwa kwa mfumo wa serikali wa malipo ya kielektroniki na mabadiliko yaliyowekwa ya asilimia ya faida katika manunuzi ya umeme yaliyofanywa kupitia M-Pesa.

**Mchango wa Mapato (Sh bilioni)**



Tukio la kusikitisha hasa mwaka huu ilikuwa kukamatwa mnamo mwezi April 2019 kwa viongozi kadhaa wa ngazi ya juu wa Vodacom Tanzania, ikiwa ni pamoja na Mkurugenzi Mtendaji Hisham Hendi, kuhusiana na tuhuma za wateja za kutumia kinyume cha sheria vifaa vya mtandao. Wafanyakazi hawa walishtakiwa kwa makosa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na makosa ya uhujumu uchumi yasiyokuwa na dhamana kulingana na Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi ya Tanzania. Baada ya kukiri kutenda makosa ya kuisababishia mamlaka husika kukosa fedha na kuruhusu matumizi ya huduma za mtandao kinyume na Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Vodacom Tanzania ilifanikiwa kuachiliwa kwa wafanyakazi wake, kwa kulipa faini ya Shilingi milioni 30 na vilevile Shilingi bilioni 5.3 kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania kama fidia kutokana na hasara za kifedha ilizopata. Ingawa makosa hayo yameelezwa wazi ndani ya sheria, ilikuwa inasikitisha kuona ukubwa wa adhabu na namna ambavyo ilitolewa. Ili kudumisha viwango vya juu kabisa vya uaminifu katika biashara, maadili na utawala bora wa shirika na kuilinda Kampuni na wafanyakazi wake kutokana na hatari za siku zijazo, tumebakiza huduma za kampuni ya uwakili ya kimataifa ili isaidie uchunguzi wa ndani ili kubaini mambo natafuta neno mbadala na kutekeleza hatua zozote zinazotakiwa kurekebisha. Timu ya Bodi ya wakurugenzi inaendelea kushirikiana na mamlaka katika suala hili.

**Malipo ya Serikali**
Sh trilioni 1.1 katika miaka 3 iliyopita



| | | |
|---|---|---|
| ■ | Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) | 88% |
| ■ | TCRA | 9% |
| ■ | UCSAF | 1% |
| ■ | Mifuko ya Hifadhi ya Jamii | 1% |
| ■ | Serikali za Mitaa | 1% |

Jukumu langu kama Mwenyekiti ni kuhakikisha kuwa Bodi, inafanya kazi ya utumishi kwa ufanisi, kusimamia utendaji wa kampuni na mwelekeo wa kimkakati na kuhakikisha kuwa timu ya uongozi inatimiza wajibu wake wa uaminifu na kijamii. Katika kutimiza jukumu hili, ninaamini kuwa tuna bahati kuwa na Bodi ambayo inakutanisha watu wenye ujuzi wa aina mbalimbali, uzoefu na mawazo yanayohitajika ili kudumisha utamaduni thabiti wa uwajibikaji. Baada ya kufanya kazi pamoja kwa miaka miwili tuna data ya kutosha kutathmini kiwango ambacho Bodi imetimiza majukumu yake. Hivi karibuni tumekamilisha mchakato wa tathmini ya ndani ya upitiaji na tutakuwa tunatekeleza hatua tulizokubaliana ili kuendelea kuimarisha na kuboresha shughuli zetu za utawala.

Kufuatia uamuzi katika Mkutano Mkuu wa Mwaka jana kupitisha gawio la juu la Sh 17.33 kwa kila hisa, na kulingana na sera ya gawio ya Kampuni kulipa angalau 50% ya mapato baada ya makato ya kodi (kutegemea masharti fulani), mwaka huu Bodi itapendekeza gawio la mwisho la Sh 24.31 kwa kila hisa. Malipo haya ya gawio ni matokeo ya utendaji thabiti wa Kundi, na yanaakisi ubora wa wafanyakazi wa Kampuni, uimara wa mkakati wake na uwezo wake kutekeleza mkakati huo. Ninaamini kuwa Kundi hili liko vizuri sana katika kuendelea kutoa thamani kwa wanahisa wake na jamii pana ya Tanzania, iliyojengwa na ongezeko la watumiaji wa huduma ya data na M-Pesa. Ongezeko hili litaungwa mkono na Kampuni kuendelea kuwekeza katika mtandao wake wa huduma ya data na majukwaa ya TEHAMA, ubora wa huduma kwa wateja wake na kina cha timu yake ya uongozi yenye vipaji na utamaduni wa ubunifu.

Kwa niaba ya Bodi, ninapenda kutoa shukrani zetu kwa timu ya uongozi wa Vodacom Tanzania na wafanyakazi wote wa Kampuni hii kwa kujitolea na kujituma jambo ambalo limejenga mwendelezo wa utendaji thabiti wa Kundi. Ninapenda pia kumshukuru Hisham Hendi kwa uongozi wake maridhawa wa Kundi mwaka huu, kwanza kwa kukaimu na sasa kama Mkurugenzi Mtendaji aliyeteuliwa rasmi. Nina imani kuwa chini ya uongozi wake, Vodacom Tanzania itaendelea kutoa mchango mkubwa katika jamii ambayo inaihudumia.

**Ali A. Mufuruki**
Mwenyekiti
Tarehe 17 Julai 2019

# Ripoti ya Mkurugenzi Mtendaji

Hisham Hendi

**Huu umekuwa mwaka unaofurahisha kwa Vodacom Tanzania PLC, ambapo tumeimarisha nafasi yetu ya kuongoza kama mtandao wenye kasi zaidi nchini, tumeongeza sehemu yetu ya soko kwa idadi ya wateja na huduma za fedha kwa simu, na kuendelea kuongoza katika alama za uhamasishaji wa mtandao, tukiwa tumeacha nafasi kubwa kutoka kwa mshindani wetu anayetufuata katika huduma, thamani na ufanisi bora wa mtandao.**



Utendaji huu mzuri umefikiwa kupitia utekelezaji thabiti na makini wa mikakati yetu, kutoa matokeo mazuri ya kifedha, kukiwa na ongezeko la mapato ya huduma na EBIT kwa 5.4% na 20.3% mtawalia. Msingi wetu wa wateja uliongezeka kwa 9.6% kufikiawateja zaidi ya milioni 14.1 uliojengwa na ongezeko la 9.7% katika wateja wa M-Pesa na ongezeko la kuvutia la 7.4% katika wateja wa huduma ya data, yote yakifanya msingi muhimu kwa ajili ya kujenga thamani kwa muda mrefu.

## Mafanikio ya kutekeleza mkakati wetu

Tumefanikisha ongezeko thabiti la mapato mwaka huu katika maeneo yetu muhimu ya kuangalia kimkakati, huduma ya data na M-Pesa, wakati mapato ya huduma ya data yakiongezeka kwa 17.9% na mapato ya M-Pesa yakiongezeka kwa 14.5%. Hatua zetu madhubuti za kurekebisha hali ya kushuka kwa mapato ya huduma ya sauti zilithibitika kuwa na mafanikio, kwa mapato ya huduma ya sauti kushuka kidogo kwa 1.1% licha ya kuendelea kuwepo kwa shinikizo la bei, ambalo liliongezeka kutokana na kupungua kwa viwango vya kuunganisha simu.

Mtazamo wetu kimkakati kuhusu kuuza data na kuleta urahisi wa huduma za kidigitali unaleta matokeo, kukiwa na ongezeko la matumizi ya huduma za data kwa 34.2%; watumiaji wa huduma ya data ya 4G waliongezeka kwa 112.0%, wateja wa data sasa wanafikia 55.8% ya jumla ya wateja wetu. Ongezeko la matumizi ya data, wateja na mapato linaakisi utendaji wetu thabiti mwaka huu katika kupanua mtandao wetu wa 4G, kuhamasisha matumizi ya simu janja, kuuza data kwa kutoa ofa mbalimbali, na kuboresha matumizi ya data kwa watumiaji wetu. Tumewekeza Sh bilioni 171.4 (16.7% ya mapato) katika mtandao wetu mwaka huu, kuongeza eneo la huduma ya 4G katika miji mikubwa, kuongeza uwezo, na kuboresha mtandao ili uweze kutoa huduma bora za data. Kufuatia kununua 700 MHz spektra katika mnada wa Juni 2018, na kutegemea mafanikio ya uzinduzi wa huduma zetu za kibiashara za 4G jijini Dar es Salaam mwaka 2017, mwaka huu tumeongeza minara 322 ya 4G, na kufanya kuwa na jumla ya minara 861 ya 4G yanayohudumia miji mikubwa na mikoa 23, na kuendelea kuongoza katika huduma ya 4G kufikia 23% ya watu nchini. Pia tumeboresha mtandao wetu, kwa kuwekeza katika kuongeza uwezo katika minara yetu ya 3G, na vilevile kuongeza minara 197 ya 3G, kufanya jumla kufikia minara 2 429. Kampeni yetu ya ubia wa simu janjja, ikiunganishwa na mtazamo wetu kuhusu makundi ya vijana na wateja wa thamani kubwa, imesababisha ongezeko la 12.6% katika watumiaji wa simu janja, kufikia kuhudumia 30.3% ya wateja wetu.

Huduma yetu ya fedha kwa simu, M-Pesa, inaendelea kuwa habari ya mafanikio, ya kuleta thamani kijamii na kifedha. M-Pesa imeongeza ushirikishaji kifedha na imehamasisha shughuli za kiuchumi kote Tanzania, wakati ikitumika kama kichocheo muhimu cha mapato na heshima kwa Kampuni. Tuna zaidi ya wateja milioni 7.0 kwa siku 30 wa M-Pesa, wanaohudumiwa na wakala 106 000, kukiwa na takribani Sh bilioni 100 za thamani ya miamala inayopitia M-Pesa kila siku. Tumeona ongezeko kubwa mwaka huu katika huduma yetu ya 'Lipa kwa M-Pesa', ambayo inawapatia

wateja uwezo wa kufanya malipo kama kituo cha huduma. Jukwaa hili limeenea katika soko la Tanzania, na kuwawezesha wateja kulipa kupitia M-Pesa kwa wafanyabiashara zaidi ya 11 000, na kuizidi idadi ya kadi za malipo nchini kote, na kufanya miamala ya Sh trilioni 1.1 katika mwaka, ikiwa ni ongezeko la 186.0%.

Tumetimiza mwaka wa tatu wa utendaji mzuri katika kuongeza mapato ya biashara na kuongeza wigo wa utoaji wa huduma zetu katika huduma ya data ya sauti, na simu zenye waya. Tumepanua kituo chetu cha cloud na data kutoa huduma na kuona ongezeko linaloridhisha katika kubisharisha huduma zetu za Intaneti ya Vitu (IoT), kupata akaunti hesabu kubwa katika usimamizi wa mnyororo tuli, smart metering, vifaa vya kuuzia vilivyounganishwa katika magari na simu, na vilevile kuleta ongezeko la majukwaa ya huduma kwa Wakulima na M-Health kwa ushirikiano na Mezzanine.

Kutokana na mazingira ya ushindani mkubwa, ilikuwa inafurahisha sana kuona ongezeko la mrejesho chanya wa kiwango cha ubora wa huduma zetu ('NPS'). Mwaka huu tumefanikiwa wakati wote kupata alama za juu za NPS kiasi cha 58, na kumaliza mwaka kwa kuongoza kwa alama 12- juu ya mshindani wetu wa karibu. Hii inaonyesha ubora wa mtandao wetu na jukwaa la huduma ya M-Pesa, athari ya uhamasishaji wetu wa 'thamani ya fedha', na uthabiti wa juhudi za kuwashirikisha wateja.

Katika kutimiza lengo letu la kuwa mtoa huduma mwenye miundombinu yenye ufanisi zaidi nchini Tanzania, tumedumisha mtazamo imara mwaka huu katika kupunguza ongezeko la gharama na kuchochea ufanisi wa kiuendeshaji kupitia programu yetu ya 'Fit for growth'. Shughuli zetu zenye ufanisi zikisaidiwa na ongezeko kubwa la 20.3% katika EBIT kukiwa na kiwango cha 11.2%, kupanua 1.4ppts. Akiba muhimu zilipatikana kupitia kupunguza gharama zinazohusiana na mtandao, kurahisisha shughuli za kiutawala na kuongeza ufanisi katika mauzo yetu na kutoa bili kupitia kuongeza matumizi ya mitambo.

Tangu kusimikwa kwetu, tumeweka msisitizo mkubwa katika kuwavutia na kuwabakiza watu wenye vipaji bora, na tunajivunia wakati wote kutathminiwa kuwa mwajiri wa chaguo. Mwaka huu tumelenga kuwabaini na kuwavutia watu wenye vipaji kutoka nje ya maeneo yetu ya asili ya biashara ili kuhakikisha kuwa tuna uwezo sahihi kwa shughuli zetu mpya za kibiashara, ikiwa ni pamoja na sayansi ya data, kujifunza mashine na michakato nyumbufu. Kama sehemu ya kichocheo chetu kuwa kampuni inayoendeshwa kidigitali, tulikuwa wa kwanza kufanya miamala ya kimataifa katika Vodacom Group kutumia miundo, kanuni na zana nyumbufu, ambazo tunatarajii zitachochea ubunifu na kufikia kuwa na faida za ufanisi na tija.

## Mazingira magumu ya uendeshaji

Utendaji wetu unaoridhisha umefikiwa katika muktadha wa shinikizo la udhibiti na sera, soko lenye mazingira ya ushindani mkubwa ambalo lina baadhi ya bei ndogo zaidi za data duniani, na wepesi katika ukuaji kiuchumi kukiwa na kupungua kwa ujumla kwa matumizi ya watumiaji.

Mwaka huu tumeendelea kuona athari viwango vya mdhibiti vya ('MTR') 'glide path'; hii ilianzishwa mnamo Desemba 2017 kwa lengo la kupunguza MTR kila mwaka kutoka thamani ya kuanzia ya Sh 15.60 kupungua hadi Sh2.00 kufika Januari 2022, moja ya kiwango kidogo zaidi cha MTR duniani. Mwaka huu, MTR ilipungua kwa 33% kuanzia Januari 2019, ikiathiri vibaya ongezeko la mapato ya huduma. Kufuatia mchakato mpana wa kushughulika na mdhibiti, tumekata rufaa kwenye Tume ya Ushindani mwaka jana dhidi ya viwango hivi vipya; rufaa yetu bado inasubiri kusikilizwa. Ongezeko la mapato mwaka huu pia limeendelea kupunguzwa na kuanzishwa kwa mfumo wa malipo serikali kielektroni, na mabadiliko yasiyotarajiwa katika mipango ya kibiashara inayoongoza malipo kati ya Vodacom na Kampuni ya Ugavi wa Umeme Tanzania.

Changamoto kubwa ya kiudhibiti inahusiana na usajili kwa kutumia alama za vidole wa wateja wote, kuunganishwa na mfumo wa Vitambulisho vya Taifa. Mchakato huu ulianza mwezi Mei 2019, na unatarajiwa kukamilika kufika Desemba 2019. Tunajituma kikamilifu kuhakikisha tunafuata kikamilifu masharti haya, lakini tunatarajii kuwepo changamoto kubwa katika kukamilisha usajili kwa kutumia alama za vidole kwa wateja zaidi ya milioni 14.1 ndani ya muda huu mfupi. Hii ina athari kubwa kwa gharama na inauwezekano wa kupunguza kwa kiasi kikubwa ongezeko la wateja wetu mwaka ujao.

## Mkakati wa msimamo wetu

Tukiangalia mbele, tutaendelea kuchochea thamani ya muda mrefu ya wanahisa na kuiongoza Tanzania kupitia safari ya kidigitali kwa kutekeleza nguzo zetu sita za kimkakati, kulinganisha uchanganuzi wa data na kutenganisha, na kubadili maisha kwa njia chanya kwa kuunganishwa na teknolojia.

Tutakuwa tukijaribu kupata ongezeko thabiti la mapato data kwa kuendelea kupanua zaidi huduma ya mtandao wetu wa 4G na 3G, kuongeza vifaa janja na kuenea kwa kadi za simu za 4G kupitia kupanga bei sahihi na njia za malipo, na kuwapatia wateja sababu zaidi za kutumia data kupita kulazimisha maudhui ya majukwaa ya kidigitali. Tutaendelea kuongeza huduma kwa wateja na kuendelea kujenga utamaduni wa kumjali mteja katika biashara zetu, ikisaidiwa na uwekezaji zaidi katika makundi ya wateja wakubwa na vijana. Kupitia jukwaa letu la kisasa la CVM, tutakuwa tukisukuma mkakati wetu wa ugawaji ili kuendelea kuongeza umiliki wetu wa soko. Jitihada zetu mbalimbali za kutoa sauti zinatarajiwa kuondoa kupungua katika mapato ya huduma ya sauti.

Jukwaa letu la M-Pesa linatoa fursa nyingi za kuwa na ongezeko zaidi, hususan tunapotoa huduma ya M-Pesa kupita utumaji wa fedha kati ya mtu na mtu, uhamishaji wa fedha kujumuisha kampuni, huduma za fedha na biashara kwa simu. Mtazamo wetu mkuu utakuwa kulinganisha ongezeko la wateja, kupanua mtandao wa wakala na wafanyabiashara kuongeza njia za mapato ya M-Pesa kupitia ubia mpya, na kuongeza mfumo wa fedha kwa simu. Tutajenga kwa kutegemea kuwepo kwa soko letu linaloongoza na majukwa na kuendeleza fursa zinazohusiana na teknolojia zinazojitokeza kama vile kusoma kwa mashine, maarifa bandia na mnyororo wa njia za kusuluhisha.

Ingawa kwa sasa biashara yetu ya kampuni inaingiza kiasi kidogo cha mapato ya huduma, tunaamini mielekeo ya hivi karibuni inayotia moyo inaakisi uwezekano wake kuwa kichocheo muhimu cha ongezeko siku zijazo. Tutachochea ukubwa na kutafuta soko la hisa katika huduma zetu zisizohamishika, kufanikisha fursa za kujenga huduma zetu za cloud na hosting, na kuongeza na kubiasharisha programu za kisasa za IoT.

Jitihada hizi mbalimbali za ukuaji zitajengwa na jitihada muhimu zinazokusudia kudumisha chapa yetu imara, kuchochea ufanisi wa kiutendaji na kuhakikisha kuwa tuna ujuzi, uwezo na utamaduni sahihi ili kufikia dira ya Kundi ya kuwa kampuni inayoongoza kidigitali.

Nina uhakika kuwa mkabala huu utaendelea kuleta unyumbufu tunapojaribu katika dira yetu kufanikisha kuongoza Tanzania katika enzi za kidigitali na kubadili maisha ya watu kupitia teknolojia.

## Shukrani

Katika kufunga, ninapenda kuwashukuru wenzangu katika Bodi, timu ya viongozi, na katika kampuni kwa msaada, ushauri na kujituma kwao. Imekuwa heshima ya ajabu kufanya kazi katika mwaka wangu wa kwanza kama Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania. Ninategemea miaka ijayo itakuwa ya kusisimua tutakapokuwa tukifanya kazi pamoja kufikisha Kampuni kuwa na uwezo wa kutosha kutoa thamani kwa wadau wake wengi kwa kuiongoza Tanzania katika enzi za kidigitali na kumuunganisha kila mmoja aishi maisha bora leo na kujenga kesho iliyo bora.

**Hisham Hendi**
Mkurugenzi Mtendaji
Tarehe 17 Julai 2019

# Uhusiano na wadau

Uwezo wa Vodacom Tanzania kutoa huduma zenye thamani unategemea mchango na shughuli za wadau mbalimbali.

Jedwali hapo chini linaeleza kwa ufupi vikundi vya wadau ambao wana athari kubwa katika uwezo wa kujenga thamani; tunaonyesha mchango wao katika kujenga thamani, namna tunavyoshirikiana nao na maslahi ya msingi ya wadau yanayohusiana na shughuli za kibiashara.

## Wateja

Ununuzi wa bidhaa na huduma zetu, unachangia kama msingi wa ongezeko la mapato.

| Namna ya kuwashirikisha | Maslahi ya msingi ya wadau |
|---|---|
| - Vituo vya mawasiliano, vituo vya mauzo rejareja na kwa mtandao<br>- My Vodacom app, USSD, chaneli za kujisaidia, M-Pesa app<br>- Net promoter score (NPS), mahojiano kufapa mrejesho, vikundi lengwa<br>- Mawasiliano ya mitandao ya kijamii<br>- Tovuti ya Vodacom Tanzania | - Ofa za thamani bora<br>- Mitandao yenye kasi kubwa na eneo pana la mtandao<br>- Kufanya iwe rahisi kuwasiliana nasi na kwa haraka zaidi<br>- Programu zilizoandaliwa kwa wateja wafanyabiashara<br>- Kutunza siri za taarifa za mteja<br>- Mrejesho kutolewa kwa masuala yanayohusiana na huduma |

## Serikali na wadhibiti

Kuwezesha kupata spektra na leseni za uendeshaji, ikiwa ni msingi wa kujenga thamani.

| Namna ya kuwashirikisha | Maslahi ya msingi ya wadau |
|---|---|
| - Kushiriki katika mikutano ya umma<br>- Kujishughulisha katika kuandaa kanuni na sheria<br>- Uchapishaji wa makala za matumizi ya sera<br>- Kushirikiana katika programu muhimu katika elimu jumuishi, ukuaji jumuishi katika kilimo na hatua jumuishi ya vita dhidi ya mabadiliko ya tabianchi | - Kuhakikisha spektra inasimamiwa kama rasilimali ya kimkakati<br>- Kufuata sheria katika masuala kama usajili wa wateja, viwango vya maingiliano ya simu, ubora wa huduma, bei, usalama, uhakika, ufanisi kiafya na kimazingira<br>- Kukuza fursa kwa maendeleo ya kiuchumi<br>- Kuchangia katika kodi |

## Wawekezaji na wanahisa

Kutoa mtaji wa fedha unaohitajika ili kuiendeleza na kukua.

| Namna ya kuwashirikisha | Maslahi ya msingi ya wadau |
|---|---|
| - Mawasiliano ya wawekezaji, ikiwa ni pamoja na makongamano na mikutano<br>- Siku za wawekezaji<br>- Matokeo ya pamoja ya mwaka na ya muda<br>- Kutoa taarifa za biashara kila robo mwaka<br>- Mkutano Mkuu wa Mwaka | - Taratibu makini za kusimamia masuala ya hatari na fursa na kuhakikisha ukuaji kifedha<br>- Kutumia taratibu nzuri za uongozi wa shirika<br>- Utoaji wa ujira kwa viongozi wa juu kwa uwazi<br>- Malipo bora ya hisa<br>- Sera madhubuti ya kutoa gawio |

## Wafanyakazi

Ujuzi na ushiriki wao huamua uwezo wetu kufanikisha dira yetu.

| Namna ya kuwashirikisha | Maslahi ya msingi ya wadau |
|---|---|
| Tovuti ya ndani<br>Vijarida, magazeti na mawasiliano kielektroniki<br>Simu ya mwajiriwa<br>Maonyesho ya uongozi | Fursa za kujiendeleza<br>Ujira wa kiushindani<br>Kubadilishana ujuzi zaidi ndani ya Kundi<br>Kujenga uwezo wa kufundisha kwa viongozi<br>Kuwa na uelewa bora wa miundo ya utoaji tuzo |

## Wasambazaji

Huathiri uwezo wetu kutoa bidhaa na huduma.

| Namna ya kuwashirikisha | Maslahi ya msingi ya wadau |
|---|---|
| Kufanya mikutano ya wasambazaji<br>Kutembelea maeneo ya biashara<br>Kufanya ukaguzi | Kulipa kwa wakati na masharti halali<br>Michakato ya zabuni iliyo wazi na ya haki<br>Kuboresha viwango vya afya na usalama |

## Jamii

Kuimarisha masuala ya kijamii na kiuchumi.

| Namna ya kuwashirikisha | Maslahi ya msingi ya wadau |
|---|---|
| Kuushirikisha umma pale vituo vya msingi vinapohitajika<br>Vodacom Foundation kushirikiana na jamii | Kupata huduma za simu za sauti na data na huduma kama vile za kifedha, kiafya na kielimu<br>Mitandao ya bure ya kijamii, elimu na kazi<br>Upanuzi makini wa miundombinu |

## Wabia wa kibiashara

Walinzi wa nembo yetu na muhimu katika kuongeza wateja.


| Namna ya kuwashirikisha | Maslahi ya msingi ya wadau |
|---|---|
| Kutembelea maduka makubwa, wakala na wauza rejareja<br>Mikutano ya kibiashara ana kwa ana<br>Mafunzo kuhusu bidhaa na huduma mpya | Kutenda haki<br>Uongozi wa juu kujishughulisha na wateja<br>Kufanya iwe rahisi na haraka kushughulika nasi |

## Vyombo vya habari

Kutoa taarifa za maendeleo ya biashara, na athari za shughuli zetu.

| Namna ya kuwashirikisha | Maslahi ya msingi ya wadau |
|---|---|
| Kuwasiliana ana kwa ana na kwa njia ya simu<br>Kufanya usaili na viongozi wakuu watendaji<br>Habari katika vyombo vya habari<br>Majadiliano<br>Uzinduzi wa bidhaa | Kupewa taarifa za shughuli muhimu na ofa mbalimbali<br>Uwazi katika utendaji<br>Ushahidi wa utendaji makini katika biashara |


# Ufanisi wetu kifedha



| Taarifa za Jumla, | Mwaka ulioishia Machi 31 2019 | 2018 | % ya mabadiliko mwaka hadi mwaka 17/18 |
|---|---|---|---|
| Mapato ya huduma (TZs m) | **1 018 910** | 966 275 | 5.4 |
| Ambapo | | | |
| Mapato ya mawasiliano ya sauti kwa simu ya mkononi (TZs m) | **388 171** | 392 294 | (1.1) |
| Mapato ya huduma ya M-Pesa (TZs m) | **333 519** | 291 193 | 14.5 |
| Mapato ya data za simu (TZs m) | **167 016** | 141 610 | 17.9 |
| Mapato ya simu zinazoingia (TZs m) | **65 709** | 82 368 | (20.2) |
| Mapato ya ujumbe mfupi (TZs m) | **41 441** | 31 571 | 31.3 |
| Jumla ya Mapato (TZs m) | **1 023 763** | 977 994 | 4.7 |
| Mapato kabla ya riba, kodi na uchakavu (EBITDA) (TZs m) | **287 879** | 266 370 | 8.1 |
| Kiwango cha EBITDA (%) | **28.1** | 27.2 | 0.9ppts |
| Mapato kabla ya riba na kodi (EBIT) (TZs m) | **114 905** | 95 509 | 20.3 |
| Kiwango cha EBIT (%) | **11.2** | 9.8 | 1.4ppts |
| Gharama za uwekezaji[1] (TZs m) | **171 432** | 159 705 | 7.3 |
| Matumizi ya mtaji kama asilimia ya mapato (%) | **16.7** | 16.3 | 0.4ppts |
| Soko letu la wateja[2] | **32.4** | 31.9 | 0.5ppts |
| Wateja hai/amilifu[3] (maelfu) | **14 133** | 12 899 | 9.6 |
| Wateja hai/amilifu wa M-Pesa kwa siku 30[4] (maelfu) | **6 989** | 6 369 | 9.7 |
| Wateja hai/amilifu wa data[5] (maelfu) | **7 892** | 7 345 | 7.4 |
| Dakika zinazotumika kwa mwezi[6] | **172** | 163 | 5.5 |
| Wastani wa kipato kwa mteja ARPU[7] (Shilingi kwa mwezi) | **6 027** | 6 086 | (1.0) |
| Idadi ya wafanyakazi | **548** | 537 | 2.0 |
| Idadi ya minara | **3 025** | 2 987 | 1.3 |
| 4G | **861** | 539 | 59.7 |
| 3G | **2 429** | 2 232 | 8.8 |
| 2G | **3 024** | 2 951 | 2.5 |
| Wingi wa NPS[8] (nafasi ikilinganishwa na washindani) | **Kwanza** | Kwanza | |

**Maelezo:**

1. Matumizi ya mtaji kama asilimia ya mapato.
2. Ripoti za Takwimu za Mawasiliano kila Robo Mwaka, Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania (TCRA)
3. Walaji wanaotumia huduma wanatokana na jumla ya idadi ya watumiaji simu waliotumia huduma yoyote katika miezi mitatu iliyopita. Hii ni pamoja na wateja wanaolipa ada ya kila mwezi ambayo inawapa haki ya kutumia huduma husika hata kama kiuhalisia hawaitumii huduma hiyo na wale wateja ambao wanawasiliana nje ya mtandao.
4. Wateja wa M-Pesa wanaotumia huduma hii ni idadi ya wateja wa kipekee ambao wamefanya miamala inayolipiwa katika siku 30 zilizopita.
5. Watumiaji wa data wanatokana na idadi ya watumiaji wa kipekee wanaozalisha data zinazowekewa bili katika mwezi. Pia wanajumuishwa watumiaji katika mipango ya pamoja ya bei, au ambao wanapata APN za shirika na watumiaji ambao wamewekewa data inayozalisha mapato ya bando katika mwezi huo. Mtumiaji anafasiliwa kuwa mtumiaji hai kama analipa ada ya mwezi ya mkataba kwa huduma hii au ametumia huduma hii katika mwezi unaoripotiwa.
6. Dakika za matumizi kwa mwezi hukokotolewa kwa kugawa wastani wa dakika kwa mwezi katika kipindi na wastani wa watumiaji halisi kwa mwezi katika kipindi hicho.
7. ARPU hukokotolewa kwa kugawa wastani wa mapato kwa mwezi na wastani wa watumiaji halisi katika kipindi hicho.
8. Net Promoter Score (NPS) ni kielezo kuanzia -100 hadi 100 ambayo inapima utayari wa wateja kupendekeza bidhaa au huduma za mtoa huduma kwa wengine. Inatumika kama kiwakilishi kwa ajili ya kupima hali ya jumla ya kuridhika kwa wateja na bidhaa au huduma ya mtoa huduma na uaminifu wa wateja kwa nembo. Kwa kila mtoa huduma, majibu hukusanywa kutoka kwa wateja ambao hutumia bidhaa au huduma zake kama njia ya msingi au mbadala wa mawasiliano ya simu. Majibu kutoka kwa watumiaji wakuu au mbadala hupimwa na uwiano wa asili wa watumiaji wakuu au mbadala kwa mtoa huduma huyo ili kukokotoa vipimo vya NPS.



## Utendaji wetu 2019

- **Mapato ya huduma** yameongezeka kwa 5.4% (7.3% ukiondoa athari za viwango vya maingiliano ya mitandao) hadi kufikia Sh bilioni 1 018.9, yakisaidiwa na ongezeko la kuridhisha la mapato ya huduma ya M-Pesa, data za simu na ujumbe mfupi. Tumefanikiwa kulinda na kuongeza idadi ya wateja wetu kutokana na msukumo wetu wa kibiashara na jukwaa la kisasa la CVM, ambapo pamoja na mkakati wetu wa mlengo wa pwani, vimechangia katika ongezeko la 9.6% katika idadi ya wateja wetu kufikia zaidi ya wateja milioni 14.1.
- **Mapato** ya jumla yaliongezeka kwa 4.7 hadi kufika Sh bilioni 1023.8, kimsingi kutokana na ongezeko la mapato ya huduma. Hali hii ilisawazishwa na mapato kidogo ya mitambo ikiwa ni matokeo ya kutekeleza mauzo ya vifaa vipya kwa kumtegemea msambazaji kwa kutumia mtu wa tatu kwa kusudio la kupanua usambazaji wa vifaa vya simu.
- **Mapato ya huduma ya sauti katika simu** yamebaki kuwa nyumbufu, yalipungua kwa 1.1 tu hadi Sh bilioni 388.3 kutokana na shinikizo la ushindani katika upangaji bei. **Dakika za kutumia** ('MoU') kwa mwezi ziliongezeka kwa 5.5, ikisaidiwa na ofa binafsi za sauti kupitia huduma yetu ya 'Ya kwako tu'.
- **Mapato ya M-Pesa** yaliongezeka kwa 14.5% hadi Shilingi bilioni 333.5, yakiwa ni matokeo ya ongezeko la wateja wetu na ongezeko la watumiaji wa bidhaa mbalimbali za huduma za fedha kwa simu – kama vile 'Pesa ni M-Pesa' – na undelezaji wa mfumo wa kiekolojia. Ongezeko hili lilifikiwa licha ya kuwepo shinikizo la kiushindani na utekelezaji wa serikali kuweka mfumo wa malipo ya serikali, ambao kwa kiasi kikubwa umepunguza mapato ya ada kutokana na manunuzi ya umeme kwa watoa huduma. M-Pesa kwa sasa inachangia 32.7% ya mapato ya huduma (ongezeko la 2.6ppt). Kwa wastani Sh trilioni 4.1 zilishughulikiwa kupitia mfumo wetu wa M-Pesa na kuongezeka kwa 16%. Bidhaa zetu mbalimbali za pesa kwa simu, zikiungwa mkono na mtandao mpana wa wakala wa usambazaji, mfumo wa M-pesa na huduma bora za wateja, yamesababisha kuwa na NPS thabiti. Huduma yetu ya 'Lipa kwa M-pesa' imeendelea kuongezeka, ikiwa na zaidi ya wafanyabiashara 11 000 wanaofanya mauzo kupitia mfumo huu.

  **Mapato ya huduma ya data** yanaendelea kuongezeka kwa 17.6%, hadi kufanikiwa kupata mapato ya Sh bilioni 167.0, kimsingi yakichangiwa na ongezeko la wateja wa data kwa 7.4% hadi milioni 7.9; wateja wa data sasa wanawakilisha 55.8% ya wateja wetu. Matumizi ya data yameongezeka kwa 34.2% kukiwa na ongezeko kubwa la matumizi ya 4G ikiakisi mahitaji makubwa ya huduma za data za simu. Mtazamo wetu kwa vijana na kundi la wateja wanaothaminiwa zaidi, ikichangiwa na ubia unaoongozwa na kampeni ya simu janja, ilisababisha kuwepo kwa mahitaji ya huduma ya mobile data kuongeza kasi na kupenyeza kwa simu janja ilisababisha ongezeko la 12.6% katika watumiaji wa simu janja, na kufikia 30.3% (juu 0.8ppt) la wateja wetu.
- **Mapato ya simu zinazoingia** yalishuka kwa 20.2% kufika Shilingi bilioni 65.7, yakiwa ni punguzo la 33.3% ya viwango vya uunganishaji wa simu (MTR) mnamo Januari 2019, hii kwa kiasi fulani ilisawazishwa na ongezeko la 22.3% la idadi ya dakika za simu zinazoingia kwa kuwa waendeshaji waliendelea kuongeza thamani bando zao za mitandao yote. Tunaendelea kuona hali ya kushuka kwa mapato ya simu zinazoingia katika mapato ya huduma, kwa sasa kwa 6.4% (pungufu 2.1ppt).
- **Mapato ya ujumbe mfupi** yaliongezeka kwa 31.3% hadi Shilingi bilioni 41.4, idadi za ujumbe mfupi zilizotumwa zilipungua kwa 11.2% hadi kufika Shilingi bilioni 34.3 wakati bei ya ujumbe mfupiiliongezeka kwa 34.1%. Hii ni kutokana na kuanzishwa kwa bando za Ujumbe Mfupi tu mwaka uliopita na uboreshaji wa mauzo ya bando hizi.

## Gharama

- **Gharama za jumla** ziliongezeka kwa 3.5% hadi Shilingi bilioni 743.0 (ukiondoa adhabu gharama za jumla ziliongezeka kwa 2.8% hadi Shilingi 737.7). Programu yetu ya kupunguza gharama iliendelea kuleta matokeo mazuri kutokana na akiba iliyopatikana, ikiendelea kusaidiwa na gharama ndogo za kuunganisha mawasiliano ya mitandao mbalimbali kutokana na kupungua gharama za maingiliano ya mitandao (MTR) pamoja na gharama ndogo za mauzo ya vifaa kutokana na kutumia vifaa vipya. Gharama hizi zilifidiwa na gharama kubwa za uendeshaji wa mitandao, kutokana na vipengele vikubwa vya mtandao na marekebisho ya ongezeko la gharama yaliyotumika chini ya mikataba ya huduma.

## Mapato kabla ya riba na kodi (EBIT)

- **Mapato kabla ya riba na kodi (EBIT)** yaliongezeka kwa 20.3% hadi Shilingi bilioni 114.9 na kusababisha EBIT kukua kwa 11.2% sawa na ongezeko la pointi 1.4. EBIT inajumuisha gharama za uchakavu za Shilingi bilioni 165.8 sawa na ongezeko la 0.8% kutokana na uwekezaji wa ziada.

## Matumizi ya mtaji


- **Matumizi ya mtaji** yalikuwa Shilingi bilioni 171.4, sawa na 7.3% au 16.7 ya mapato. Uwekezaji wetu ulilenga kuongeza uwezo wa mtandao wa data na kuongeza maeneo ya huduma ya 4G katika miji mikubwa. Minara mipya 322 zaidi ilifungwa pamoja na mkongo wa taifa ili kuongeza watumiaji wa data kuimarisha nafasi ya kuwa mtandao unaoongoza kwa kasi zaidi nchini. Pia tumeboresha mtandao wetu kwa kuendelea kuboresha minara ya 3G na vilevile kuongeza idadi ya minara ya 3G 197kufikia minara 2 429.

1. Hii haijumuishi gharama za uchakavu na gharama zitokanazo na malipo ya hisa.
2. Gharama ya jumla ya adhabu ya Sh bilioni 5.3 iliyofuatia maamuzi ya Mahakama.
3. Ookla speed test report as at 31 March 2019.

# Viongozi wetu

Tuna Bodi yenye wakurugenzi 12, wengi wao ni wakurugenzi wasio watendaji. Mwenyekiti wetu ni mkurugenzi asiye mtendaji.

## Muundo wa Bodi




**1. Ali A. Mufuruki** (60)
Aliteuliwa Agosti 2017
- Uzoefu mkubwa wa uongozi
- Mtaalamu wa uongozi wa shirika
- Mahusiano na serikali

**2. Hisham Hendi** (39)*
Aliteuliwa Machi 2019
- Kiongozi mwerevu wa biashara
- Uzoefu wa masoko anuwai yanayoibukia
- Utekelezaji madhubuti wa ubunifu wa bidhaa na matoleo mapya

**3. Jacques Marais** (53)
Aliteuliwa Julai 2016
- Ujuzi wa kutosha wa masuala ya fedha
- Uzoefu mkubwa wa masoko yanayoibuka
- Ujuzi mkubwa wa masuala ya mawasiliano ya simu

**4. Andries Daniel Jan Delport** (55)
Aliteuliwa Aprili 2015
- Maarifa na uzoefu mkubwa katika teknolojia ya mawasiliano ya simu
- Utaalamu wa uongozi wa kimkakati
- Utaalamu wa uendeshaji na utekelezaji wa mikakati

**5. Margeret Ikongo** (62)
Aliteuliwa Novemba 2017
- Utaalamu wa fedha
- Uhusiano na serikali
- Utaalamu wa uongozi wa shirika

**6. Kenneth Kwame Gomado** (41)
Aliteuliwa Machi 2018
- Uzoefu wa masoko anuwai yanayoibuka ya kifedha
- Ujuzi mkubwa wa mawasiliano ya simu na FMCG
- Uzoefu wa ushauri wa masuala ya ukaguzi

**7. Diego Gutierrez** (44)
Aliteuliwa Machi 2018
- Mpanga mikakati ya kibiashara
- Maarifa mapana kuhusu teknolojia ya simu na uzoefu wa soko linaloibuka
- Utaalamu wa uongozi wa kimkakati

**8. Matimba Mbungela** (47)
Aliteuliwa Agosti 2017
- Maarifa na uzoefu mkubwa wa usimamizi wa vipaji
- Utaalamu katika taratibu bora za kushughulikia rasilimali watu
- Uzoefu wa uendeshaji wa shughuli za kimataifa

**9. Winnie Ouko** (49)
Aliteuliwa Novemba 2017
- Mtazamo wa masoko kimkakati
- Utaalamu wa fedha
- Uzoefu wa uendeshaji na utekelezaji wa mikakati kimataifa

**10. Thembeka Semane** (43)
Aliteuliwa Novemba 2017
- Utaalamu wa utawala wa shirika
- Uzoefu wa utekelezaji wa shughuli za uendeshaji na mikakati
- Utaalamu wa fedha

**11. Henry JC Surtees** (49)
Aliteuliwa Mei 2011
- Uzoefu wa masuala ya fedha
- Utaalamu wa utawala wa shirika
- Utaalamu wa uongozi wa shirika

**12. Till Streichert (45)**
Aliteuliwa Agosti 2017
- Uzoefu mbalimbali wa masuala ya fedha kimataifa
- Historia ya uongozi wa juu
- Umaizi wa sekta ya TEHAMA kimataifa

* Bw. Hendi alichukua nafasi ya uongozi kuanzia tarehe 19 Machi, 2019. Amekuwa akifanya kazi katika wadhifa wa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji tangu Septemba 2018.

(A) Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekeleziji (R) Kamati ya Ujira

# Kamati ya Utendaji

Mkurugenzi Mtendaji

1


Masuala ya Fedha

2


Masuala ya Watumiaji/Walaji

3


Masuala ya Biashara M-Pesa

4


Shughuli za Biashara

5


Mtandao

6


Masuala ya Sheria na Kanuni

7


Masuala ya Shirika

8


Shughuli za Wateja

9


Rasilimali Watu

10


TEHAMA

11


**1. Hisham Hendi** (39)
Alijiunga Vodacom mwaka 2014, Vodafone 2003

**2. Jacques Marais** (53)
Mkurugenzi wa Fedha
Alijiunga Vodacom mwaka 2001

**3.Linda Riwa** (32)
Kaimu Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara ya Walaji
Alijiunga Vodacom mwaka 2017

**4. Epimack Mbeteni** (41)
Mkurugenzi wa Biashara – M-Pesa
Alijiunga Vodacom mwaka 2014

**5. Arjun Dhillon** (39)
Mkurugenzi Kitengo cha Shughuli za biashara
Alijiunga Vodacom mwaka 2017, Safaricom 2015

**6. Alec Mulonga** (44)
Mkurugenzi wa Mtandao
Alijiunga Vodacom mwaka 2012

**7. Olaf Mumburi (43)**
Mkurugenzi masuala ya Kisheria na Kikanuni
Alijiunga Vodacom mwaka 2008

**8. Rosalyn Gloria Mworia** (39)
Mkurugenzi wa masuala ya Shirika
Alijiunga Vodacom mwaka 2008

**9. Harriet Atweza Lwakatare** (41)
Mkurugenzi wa huduma kwa wateja
Alijiunga Vodacom mwaka 2012

**10. Vivienne Penessis** (44)
Mkurugenzi Rasilimali Watu
Alijiunga Vodacom mwaka 2018

**11.Luis Fedriani** (47)
Mkurugenzi wa TEHAMA
Alijiunga Vodacom mwaka 2012

# Wafanyakazi wetu

Jumla ya wafanyakazi
548
(2018: 537)

Wanawake
38%
(2018: 39%)

Wanaume
62%
(2018: 61%)

# Tamko la utekelezaji

Vodacom Tanzania Public Limited Company (Vodacom Tanzania) inajituma kwa viwango vya juu zaidi vya uaminifu, maadili na utaalamu wa biashara.

Kanuni za utawala wa shirika zinajumuisha nidhamu, uhuru, uwajibikaji, utendaji haki, uwajibikaji kwa jamii, uwazi na uwajibikaji wa wakurugenzi kwa wadau wote. Kanuni hizi zimeimarishwa katika taratibu za udhibiti wa ndani na sera za Vodacom Tanzania zinazoongoza utendaji katika shirika na zimeoanishwa na miongozo ya Mamlaka ya Masoko ya Mtaji na Dhamana kuhusu taratibu za utawala wa shirika zinazofanywa na kampuni za umma zilizoorodheshwa nchini Tanzania.

## Muundo wa utawala wa shirika

Ufuatao ni muundo wa utawala wa Vodacom Tanzania hadi kufika tarehe 31 Machi 2019.

### BODI
Kamati za Bodi

- Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji
- Kamati ya Ujira na Uteuzi

### MKURUGENZI MTENDAJI
Kamati ya Utendaji

- Fedha
- Kitengo cha Biashara ya walaji
- Kitengo cha Biashara – Mpesa
- Kitengo cha Biashara ya Kampuni
- Mtandao
- Sheria na Kanuni
- Masuala ya Shirika
- Kushughulikia Wateja
- Rasilimali Watu
- TEHAMA

## Uongozi wa kimaadili

Bodi inakubali kuwajibika kwa pamoja kwa kueleza namna maadili na tabia za kimaadili zinapaswa kutekelezwa katika Vodacom Tanzania. Hii ni pamoja na kupanga taratibu za mwenendo wa wajumbe wa Bodi, kuhakikisha kuwa wanatenda kwa uaminifu, uzoefu, kuchukua majukumu, uwajibikaji, kutenda haki na kuwa na uwazi. Sifa hizi zinaweka mwelekeo kuanzia juu ili kuunga mkono utamaduni wa kimaadili ndani ya Vodacom Tanzania.

# Uongozi wa Bodi na Kamati Mbalimbali

## Bodi

Kama sehemu ya kuorodheshwa kwetu kwenye Soko la Hisa Dar es Salaam, Bodi iliundwa kuakisi muundo mpya wa umiliki wa hisa na mfumo wa kisheria, kulingana na Sheria ya Soko la Mitaji na Dhamana, Sheria ya Makampuni, Kanuni za Soko la Hisa la Dar es Salaam na Kanuni na miongozo ya Vodacom Tanzania.

Vodacom Tanzania ina Bodi moja yenye wakurugenzi 12, ambapo wanne kati yao (pamoja na Mwenyekiti) ni wakurugenzi huru wasio watendaji, sita wasio watendaji (lakini si huru kwa kuwa wanawakilisha wanahisa wakubwa), na wawili ni wakurugenzi watendaji. Bodi imeridhika kuwa mlingano wa maarifa, ujuzi, uzoefu na uanuwai katika Bodi ni wa kutosha.

Bodi inaweza kukutana kwa ajili ya kufanya shughuli, kuahirisha na vinginevyo kudhibiti mikutano yake kama itakavyoona inafaa. Mikutano ya kawaida ya bodi hufanyika mara kwa mara kutathmini mikakati ya kibiashara, utendaji na ufanisi wa kifedha, na vilevile kufanya usimamizi. Mikutano maalum ya Bodi inaweza kufanyika wakati ikihitajika.

Kamati ya Ujira na Uteuzi mara kwa mara hutathmini upokezanaji wa uongozi ndani ya Bodi na kamati zake ili kuhakikisha tunakuwa na watu wenye ujuzi na uzoefu sahihi siku za baadaye. Mkurugenzi Mtendaji anawajibika na kuhakikisha kuwa wafanyakazi muhimu wa menejimenti wana ujuzi, mamlaka na rasilimali muhimu ili kutekeleza mkakati wa Vodacom Tanzania.

## Uwajibikaji

Bodi inabeba wajibu wa jumla kwa mafanikio ya Vodacom Tanzania. Nafasi yake ni kutoa uongozi na uamuzi wa busara katika kuelekeza Vodacom Tanzania kufikia ukuaji endelevu na kutenda kwa mslahi makubwa ya wanahisa wake.

Kulingana na taratibu za uongozi bora, nafasi za Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji zinatofautiana. Mwenyekiti anawajibika kuongoza Bodi, wakati Mkurugenzi Mtendaji anawajibika na uendeshaji wa menejimenti ya Vodacom Tanzania.

Katiba ya Bodi inaeleza wajibu wa Bodi, ambao unajumuisha:

- Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji na Mkurugenzi wa Fedha;
- Usimamizi makini wa mwelekeo wa kimkakati wa Vodacom Tanzania;
- Kuidhirisha miradi inayohitaji mitaji mikubwa, ununuzi au uuzaji wa hisa;
- Kufanya uamuzi wenye manufaa kuhusu masuala ya biashara ya Vodacom Tanzania; mbali na menejimenti;
- Kuhakikisha kuwa vyombo sahihi vya utawala, sera na taratibu zimewekwa;
- Kuhakikisha kuwa vyombo sahihi vya utawala, sera na taratibu zimewekwa;
- Kuhakikisha kunakuwa na ufanisi katika udhibiti wa ndani wa Vodacom Tanzania;
- Kupitia na kutathmini viashiria hatarishi kwa Vodacom Tanzania;
- Kupitisha bajeti ya mwaka na mpango wa uendeshaji;
- Kupitisha matokeo ya pamoja ya mwaka nay a muda fedha na vilevile mawasiliano yote na wanahisa;
- Kupitisha muundo wa viongozi wa juu, wajibu na mpango wa kupokezana madaraka; na
- Usimamizi wa habari na teknolojia.

## Wakurugenzi

Kanuni za kampuni ya Vodacom Tanzania zinaeleza kuwa wakurugenzi wote wanastahili kustaafu kwa kupokezana na wanaweza kuchaguliwa tena na wanahisa angalau mara moja kila baada ya miaka mitatu.

## Mwenyekiti

Kanuni za kampuni zinaitaki Bodi kumchagua Mwenyekiti kila mwaka. Bodi inaridhika kuwa Mwenyekiti anaweza kutekeleza majukumu ya nafasi hii kwa ufanisi. Bw. Ali A. Mufuruki aliteuliwa kama Mwenyekiti wa Vodacom Tanzania kuanzia siku ya Jumatano tarehe 17 Julai 2019. Kuchaguliwa kwake tena kama Mwenyekiti kutazingatiwa na Bodi wakati atakapotimiza mwaka mmoja.

## Ushauri huru

Bodi inatambua kuwa inawezekana kukawepo matukio ambapo wakurugenzi wanachukulia ni muhimu kuchukua ushauri huru wa kitaalumu. Hili hufanyika kwa gharama za Vodacom Tanzania, kulingana na taratibu zilizokubaliwa.

# Shughuli za uongozi wa kampuni

## Mikutano ya Bodi

Bodi hufanya mikutano isiyopungua mitatu kila mwaka. Mikutano maalum ya Bodi huitishwa inapobidi. Mikutano mitano maalum ya bodi iliitishwa katika mwaka huo.

Jedwali hapo chini limerekodi mahudhurio ya wakurugenzi katika mikutano ya Bodi kwa mwaka huo.

| Jina la Mkurugenzi | 3 Mei 2018 Maalum | 17 Mei 2018 Maalum | 30 Mei 2018 | 4 Julai 2018 | 12 Julai 2018 Maalum | 13 Sept 2018 | 5 Nov 2018 Maalum | 6 Nov 2018 | 17 Jan 2019 Maalum | 5 Machi 2019 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ali A. Mufuruki (Mwenyekiti) | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Till Streichert | ✓ | X | ✓ | ✓ | X | ✓ | ✓ | ✓ | X | ✓ |
| Matimba Mbungela | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Andries Delport | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Henry Surtees | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Ian Ferrao[1] | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | R | R | R | R | R |
| Jacques Marais | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | X | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Margaret Ikongo | ✓ | ✓ | X | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Thembeka Semane | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | X | X | ✓ | ✓ |
| Winifred Ouko | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Diego Gutierrez | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | X | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Kenneth Gomado | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | X | X | ✓ | ✓ |

**Maelezo:**
1. Ian Ferrao amestaafu tarehe 1 Septemba 2018.

## Kamati za Bodi

Wakurugenzi wasio watendaji wanachangia uzoefu wao mkubwa na maarifa kwenye Kamati za Bodi.Kamati zote hufanya kazi chini mikataba iliyopitishwa na Bodi, ambayo hurekebishwa mara kwa mara ili kuenda sambamba za mabadiliko katika sheria ya makampuni na taratibu bora za uongozi.

Bodi ina Kamati ya Ujira na Uteuzi na Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji, zote mbili zina shughuli zilizokasimiwa.

Kamati za Bodi zinawajibika kufanya upitiaji na usimamizi makini wa shughuli kulingana na hadidu za rejea. Kila kamati inapaswa kuwa na wajumbe wa Bodi wasiopungua watatu au watu wengine kama Bodi itakavyoona inafaa, alimradi kuwa kamati yoyote iliyoundwa ifuate kanuni zozote itakazowekewa na Bodi na kuwa mjumbe atakuwa kwa cheo chake mjumbe wa kamati yoyote iliyoanzishwa.

## Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji

**Wajumbe:** Margaret Ikongo (Mwenyekiti), Thembeka Semane na Winifred Ouko.

Kamati hii imeundwa kwa kuzingatia utaratibu bora wa utawala. Kamati hii ina wakurugenzi huru watatu wasio watendaji. Mkurugenzi Mtendaji na Mkurugenzi wa Fedha, na vilevile mkaguzi wa nje, wanahudhuria Mikutano ya Kamati kwa mwaliko.

Jukumu la msingi la Kamati hii ni kuhakikisha ukamilifu wa utoaji wa taarifa za fedha, mchakato wa ukaguzi na kuwa mifumo ya udhibiti wa dharura na udhibiti wa ndani inadumishwa. Katika kushughulikia malengo haya, Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji inasimamia mahusiano haya na mkaguzi wa nje na kupitia ufanisi wa shughuli ya ukaguzi wa ndani.

Wakaguzi wa ndani na nje hawana kikwazo cha kumfikia Mwenyekiti wa Kamati hii. Idara ya ukaguzi wa ndani inaripoti moja kwa moja kwenye Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na pia inawajibika kwa Mkurugenzi wa Fedha kwa masuala ya utawala ya kila siku.

Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji inawajibika:

- Kupitia matokeo ya jumla ya muda, matokeo ya awali ya mwaka, ripoti ya mwaka na taarifa za fedha za mwaka za Vodacom Tanzania na kampuni zake tanzu (pamoja na Kundi la makampuni);
- Kufuatilia utekelezaji wa sheria zinazotumika na Kanuni za Soko la Mtaji la Dar es Salaam;
- Kuripoti kwenye Bodi kuhusu ubora na kukubalika kwa sera na taratibu za hesabu za fedha za Kundi la Makampuni ya Vodacom;
- Kutoa usimamizi makini wa mchakato wa kutoa ripoti ya mwaka;
- Kuzingatia uteuzi na/au kuvunja mkataba wa mkaguzi wa ndani, ada za ukaguzi, uhuru na huduma zozote zisizokuwa za ukaguzi zinazohitajika;
- Kupitisha mpango wa ukaguzi wa ndani kwa mwaka;
- Kuchukua hatua sahihi kufuatia malalamiko yoyote yaliyopokelewa, kutoka vyanzo vya ndani au nje, ambayo yanahusiana na taratibu za utunzaji wa fedha, kazi ya ukaguzi

wa ndani, ukaguzi wa nje wa Vodacom Tanzania na kampuni zake tanzu, taarifa za fedha za mwaka za Kundi la Makampuni ya Vodacom pekee na za pamoja, yaliyomo na ufichuaji zijumuishwe kwenye taarifa hizi za fedha, au jambo lolote linalohusiana;
- Kupitia na kufuatilia usimamizi na utoaji wa ripoti za masuala yanayohusiana na kodi;
- Kufuatilia kazi na michakato ya usimamizi wa dharura na kutathmini hatari muhimu zaidi za Kundi la Makampuni ya Vodacom; na
- Kufuatilia ufanisi wa michakato ya kujenga ufahamu na kujenga uelewa wa sheria na kanuni husika ili kuhakikisha zinafuatwa na menejimenti.

Mikutano ya Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji isiyopungua mitatu imepangwa kufanyika kila mwaka wa fedha. Mikutano ya ziada ya kamati inaweza kuitishwa ikibidi. Mikutano mitano maalum ilifanyika katika mwaka huo.

Jedwali hapo chini limerekodi mahudhurio ya wakurugenzi katika Mikutano ya Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji katika mwaka.

| Jina la Mkurugenzi | 3 Mei 2018 Maalum | 17 Mei 2018 Maalum | 30 Mei 2018 | 4 Julai 2018 | 12 Julai 2018 Maalum | 13 Sept 2018 | 5 Nov 2018 Maalum | 6 Nov 2018 | 17 Jan 2019 Maalum | 5 Machi 2019 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Margaret Ikongo | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Thembeka Semane | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | X | ✓ | ✓ | ✓ |
| Winifred Ouko | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |

## Kamati ya Ujira na Uteuzi

**Wajumbe:** Winifred Ouko (Mwenyekiti), Diego Gutierez, Henry Surtees na Matimba Mbungela.

Kamati ya Ujira na Uteuzi inafanya kazi ili kuwezesha na kuisaidia Bodi kutekeleza wajibu wake kwa:

- Kuamua na kukubali ujira na marupurupu ya wafanyakazi muhimu wa menejimenti, isipokuwa wafanyakazi walioazimwa;
- Kuamua, kukubali na kutunga sera ya ujira ya Vodacom Tanzania na kuhakikisha inaendana na sera ya mishahara ya Vodacom Group Limited;
- Kuhakikisha kuwa mikakati ya haki, kiushindani na programu zipo kuwezesha kuajiri, kutoa motisha na kuwabakiza wafanyakazi wenye utendaji wa hali ya juu katika ngazi zote katika kusaidia kufanikisha malengo ya shirika na kulinda maslahi ya wanahisa;
- Kupitia na kupendekeza kwenye Bodi vigezo vilivyo muhimu kupima utendaji wa wafanyakazi muhimu wa menejimenti katika kufanya kazi na wajibu wao;
- Kutunga na kutekeleza sera ya falsafa ya ujira;
- Kuzingatia manufaa au mipango mingine muhimu yenye umuhimu kifedha;
- Kupitia sera za kupandisha vyeo, kuhamisha na kuachisha kazi kwa ajili ya Vodacom Tanzania;
- Kufuatilia ukubwa na muundo wa Bodi;
- Kupendekeza watu kwa ajili ya uteuzi kama wajumbe wa Bodi na kamati zake;
- Kupitia mipango ya Bodi ya kupokezana madaraka;
- Kuhakikisha kuwa utendaji wa wajumbe wa Bodi unapitiwa upya;
- Kuamua muundo na ufanisi wa bodi za kampuni tanzu za Vodacom Tanzania;
- Kuthibitisha uteuzi wa watu kwenye bodi husika za kampuni tanzu za Vodacom Tanzania;
- Kuhakikisha uwezo wa wajumbe wa bodi;
- Kupitia muundo wa shirika ili kuhakikisha kuwa unafaa kwa madhumuni, kuwasilisha mkakati na malengo ya muda mrefu ya biashara; na
- Kuhakikisha sheria na kanuni zinazotumika zinaheshimiwa.

Jedwali lifuatalo limerekodi mahudhurio ya wakurugenzi katika mikutano ya Kamati ya Uteuzi na Ujira kwa mwaka huo

| Jina la mkurugenzi | 30 Mei 2018 | 13 Sept 2018 | 6 Nov 2018 | 8 Machi 2019 |
|---|---|---|---|---|
| Winfred Ouko | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Diego Gitierrez | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Henry Surtees | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Matimba Mbungela | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |

Kamati ya Ujira na Uteuzi imevunjwa kutengeneza Kamati mbili tofauti. Kamati ya Uteuzi ilianza kazirasmi tarehe 1 April 2019.

# Kamati ya Uteuzi na Ujira

Ripoti hii inatoa muhtasari wa falsafa na sera ya ujira ya Vodacom Tanzania kwa ajili ya wakurugenzi watendaji na wasio watendaji. Pia inatoa maelezo kuhusu namna ambavyo sera imetekelezwa.

## Barua kutoka kwa Mwenyekiti ya Kamati ya Uteuzi na Ujira

Wapendwa wanahisa,

Sehemu ya mwelekeo wetu ni kuisaidia na kuishauri Bodi kuhusu mambo yanayohusu ajira ya wakurugenzi watendaji. Tunahakikisha kuwa falsafa na sera ya ajira inasaidia malengo ya kimkakati ya Kampuni ili kuwezesha kuajiri, kutoa motisha na kudumu na watendaji kwa madhumuni ya kuongeza thamani ya wanahisa na kufuata sheria na miongozo iliyotolewa na Mamlaka ya Soko la Mitaji na Hisa.

Kamati imezingatia masharti ya kutoa taarifa ya Sheria ya Soko la Mtaji na Hisa, 1994 na imetoa ripoti ifuatayo, ambayo inafuata miongozo kuhusu taratibu za usimamizi wa shirika unaofanywa na kampuni zilizoorodheshwa kwa umma nchini Tanzania wakati tukielewa kuhusu kutoa taarifa nyeti za watu binafsi au masoko. Ninapenda kushukuru wajumbe wenzangu wa kamati kwa kuendelea kuniunga mkono na ninataraji kufanya kazi nao mwaka ujao.

**Winifred Ouko**
Mwenyekiti wa Kamati ya Uteuzi na Ujira



Kulingana na miongozo ya CMSA kuhusu taratibu za usimamizi wa shirika unaofanywa na kampuni zilizoorodheshwa kwa umma nchini Tanzania, ripoti hii inaeleza sera za Vodacom Tanzania za ujira kwa ajili ya wakurugenzi watendaji na wasio watendaji hususan wale wanaohitajika na kipengele cha ujira kwa wakurugenzi ikiwahusisha wasio wakurugenzi watendaji kwa pamoja.

### Falsafa, sera na mfumo wetu wa utoaji wa ujira kwa mwaka huu inayotumika kwa wakurugenzi watendaji

Lengo letu ni kuvutia, kubakiza na kutoa motisha kwa watendaji wa ngazi ya juu zaidi, wakati huohuo kulinganisha ujira wao na maslahi ya wanahisa na taratibu bora. Mpango wetu kutoa tuzo ni wa jumla, umelingana katika vipengele vifuatavyo:

- Uhakika wa fungu;
- Vivutio vya muda mfupi;
- Vivutio vya muda mrefu;
- Programu mbalimbali za utambuzi;
- Fursa za kujifunza na kuendelea kwa kila mtu;
- Mazingira ya kazi yanayovutia; na
- Programu ya ustawi wa wafanyakazi iliyoandaliwa vizuri na inayoingiliana.

Wakurugenzi watendaji wanafuata jumla ya gharama kwa falsafa ya kampuni, ambayo inarejelewa kama kifurushi cha uhakika. Uchangiaji katika huduma za tiba, malipo ya kustaafu na maslahi yaliyowekewa bima vimejumuishwa katika kifurushi chenye uhakika.

Vipengele hivyo hapo juu vimeungwa mkono na kuimarishwa na maendeleo ya utendaji wetu na michakato ya usimamizi wa vipaji. Sera yetu ni kuwapatia marupurupu watendaji wetu kwa michango yao katika utendaji wetu kimkakati, kifedha na kiutendaji. Kuwa mwajiri bora katika tasnia yetu tunahitaji kuwavutia, kuwaendeleza na kubakiza vipaji bora na mtaji wa wataalamu, kitaifa na kimataifa.

Kwa mwaka, huwa tunaendesha zoezi la kuweka viwango na zawadi huongezeka katika GP kulingana na soko, utendaji binafsi na uwezekano wa utendaji binafsi na tathmini inayowezekana inaamuliwa kupitia usimamizi wetu wa vipaji na michakato ya uendelezaji wa utendaji. Matokeo ya michakato hii pia huathiri utoaji wa vivutio vya muda mfupi na muda mrefu siku zijazo.

Kivutio chetu cha muda mfupi, kwa bonasi ya mwaka ya fedha taslimu, kinaunganishwa katika kufanikisha malengo ya kifedha, kimkakati na kiuendeshaji na ufanisi wa watendaji dhidi ya malengo yao. Kiwango kilichopo kwa ajili ya vivutio vya muda mfupi huamuliwa kutokana na ufanisi wa kifedha wa Kampuni dhidi ya malengo yaliyopangwa hapo awali.

Wakurugenzi watendaji ambao wameazimwa kufanya kazi na Vodacom Tanzania wanakuwa kwenye mfumo wa vivutio vya muda mrefu wa Vodacom Group Limited ambapo mgao wa hisa za mwaka za Vodacom Group Limited hutolewa na mwajiri wao husika. Hii inahimiza umiliki na uaminifu, na kuunga mkono malengo ya Vodacom kuwabakiza wafanyakazi wenye thamani. Mfumo huo ni mfumo kamili wa umiliki; matokeo yake, washiriki wanapokea magawio kutoka tarehe ya utoaji ingawa thamani ya hisa itaweza kupatikana tu baada ya kipindi cha miaka mitatu, kwa kiwango ambacho masharti ya uwekezaji yamefikiwa.

## Utoaji wa taarifa za ujira wa wakurugenzi watendaji na wasio watendaji

### Ujira wa Wakurugenzi Watendaji – Malipo ya Uhakika

Ujira kwa wakurugenzi watendaji ulipitiwa kwa kuzingatia kupanga viwango vya soko na hatari zinazohusiana na kubaki na wafanyakazi muhimu wa menejimenti.

Utoaji wa taarifa za ujira wa wakurugenzi watendaji na wasio watendaji umeonyeshwa katika Maelezo 34 (Pande husika) ya taarifa za pamoja za mwaka za fedha katika ukurasa — wa taarifa hizi za mwaka.

### Kutekeleza sera

Utoaji wa taarifa uliowasilishwa katika ripoti hii ya mwaka kuhusu tuzo kwa wafanyakazi wanaostahili ambapo maamuzi yote ya ujira yametolewa na sera ya ujira kama ilivyopitishwa awali na wanahisa. Kumekuwa hakuna mabadiliko kinyume na sera katika mwaka huu wa fedha.

# Taarifa ya Mkutano Mkuu

**Vodacom Tanzania Public Limited Company**
(Imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
(Namba ya usajili 38501)
(ISIN: TZ1996102715 Ticker code: VODA)
('Vodacom Tanzania' au 'Kampuni')

Taarifa inatolewa kuwa mkutano mkuu wa tatu wa Kampuni kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2019 utafanyika siku ya Ijumaa tarehe 20 Septemba 2019, katika Ukumbi wa Mlimani City, Mlimani City Park, Barabara ya Sam Nujoma, Dar es Salaam, Tanzania saa 4:00 asubuhi. Mkutano huu utajadili yafuatayo:

## 1. Kuthibitisha kumbukumbu

Kuthibitisha kumbukumbu za mkutano mkuu wa pili uliofanyika tarehe 1 Oktoba 2018 na mkutano mkuu wa dharura uliofanyika tarehe 14 Novemba 2018.

### Azimio la kawaida namba 1

"ILIAMULIWA KUWA kumbukumbu za mkutano mkuu wa pili uliofanyika tarehe 1 Oktoba 2018 zimethibitishwa."

### Azimio la kawaida namba 2

"ILIAMULIWA KUWA kumbukumbu za mkutano mkuu wa dharura uliofanyika tarehe 14 Novemba 2018 zimethibitishwa."

Nakala za kumbukumbu zinapatikana kwenye tovuti ya Kampuni **www.vodacom.co.tz/investor-relations**

## 2. Kupitisha taarifa za fedha za mwaka zilizokaguliwa

Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2019.

### Azimio la kawaida namba 3

"ILIAMULIWA KUWA taarifa ya fedha zilizokaguliwa za Kampuni ikijumuisha kampuni zake tanzu, pamoja na ripoti ya wakaguzi huru na ya wakurugenzi kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2019, zimepokelewa na kupitishwa."

Taarifa ya mwaka inapatikana katika tovuti ya Kampuni **www.vodacom.co.tz/investor-relations**

## 3. Uchaguzi wa wakurugenzi

3.1 Ndg. Hisham Hendi aliteuliwa kujaza nafasi iliyojitokeza katika Bodi na kuendelea kutekeleza majukumu ya kiofisi hadi mkutano wa kawaida unaofuata kulingana na ibara ya 86 ya Kanuni za Kampuni, na hivyo anastahili kuchaguliwa tena.

Ufuatao ni wasifu wa Ndg Hisham Hendi:

**Hisham Hendi (39)**
**Mkurugenzi Mtendaji – Vodacom Tanzania PLC**
*Shahada katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Cairo.*
*Vodafone's Global Leadership Program (Inspire), London Business School.*
*Cheti cha Ubora katika Biashara, Chuo cha IMD kilichopo Lausanne, Switzerland.*

Hisham aliteuliwa kuwa mkurugenzi mtendaji wa Vodacom Tanzania mnamo Machi 2019. Hisham amekuwa akifanya kazi kama Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania tangu Septemba 2018. Kabla ya hapo, Hisham alikuwa Mkurugenzi wa Kitengo cha Shughuli za Biashara cha Vodacom Tanzania tangu Agosti 2016, ambapo mikakati yake ilileta mabadiliko katika kitengo hiki na kufanikisha ukuaji mwaka hadi mwaka. Ana uzoefu wa zaidi ya miaka 15 katika masuala ya simu akiwa amefanya kazi na kushika nafasi mbalimbali za uongozi katika masoko mbalimbali ikiwemo Uingereza, Misri na Afrika Kusini.

### Azimio la kawaida namba 4

"ILIAMULIWA KUWA Ndg. Hisham Hendi amechaguliwa kuwa mkurugenzi wa Kampuni."

3.2 Ndg. Henry JC Surtees, Ndg. Till Streichert, Ndg. Ali A Mufuruki na Bi Margaret Ikongo wanastahili kustaafu katika mkutano huu mkuu kwa mujibu wa Kanuni za Kampuni namba 104 na 105. Kanuni hizo zinabainisha kuwa licha ya kustaafu, wanaweza kuchaguliwa kwa mara nyingine tena kuwa wakurugenzi.

### Azimio la kawaida namba 5

"ILIAMULIWA KUWA Ndg. Henry JC Surtees amechaguliwa tena kuwa mkurugenzi wa Kampuni."

## Azimio la kawaida namba 6

"ILIAMULIWA KUWA Ndg. Till Streichert amechaguliwa tena kuwa Mkurugenzi wa Kampuni."

## Azimio la kawaida namba 7

"ILIAMULIWA KUWA Ndg. Ali A Mufuruki amechaguliwa tena kuwa Mkurugenzi wa Kampuni."

## Azimio la kawaida namba 8

"ILIAMULIWA KUWA Bi Margaret Ikongo amechaguliwa tena kuwa Mkurugenzi wa Kampuni."

Ufuatao ni wasifu wa Ndg. HJC Surtees, Ndg. T Streichert, Ndg. AA Mufuruki na Bi M Ikongo:

### Henry JC Surtees (48)

**Mkurugenzi wa Bodi asiye mtendaji**
**Mjumbe wa Kamati ya Ujira na Uteuzi**
*Shahada ya Sayansi, Chuo Kikuu cha Durham England, Cheti cha taaluma ya Uhasibu (ICAEW) UK pamoja na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi, Tanzania.*

Henry amekuwa mkurugenzi wa Vodacom tangu Mei 2011. Pia anashikilia wadhifa wa Mkuu wa Kitengo cha Fedha, Mdhibiti Fedha na Katibu wa Kampuni ya Caspian Limited. Kabla ya kushika nafasi hii, Henry ameshika nafasi mbalimbali kama mkurugenzi, mshauri na Katibu wa Kampuni kwa biashara zingine za kitaalamu.

### Till Streichert (45)

**Mkurugenzi wa Bodi asiye mtendaji**
**Afisa Mkuu Fedha wa Vodacom Group Limited**
**Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Vodacom Group**
**Mkurugenzi asiye Mtendaji wa Vodacom SA**
**Mkurugenzi Mbadala asiye Mtendaji wa Safaricom**
*Dr. Phil. Chuo Kikuu cha Hannover, Ujerumani*

Till aliteuliwa kama mkurugenzi asiye mtendaji wa Vodacom Tanzania mnamo Novemba 2017, mkurugenzi asiye mtendaji wa Vodafone Kenya na kama mkurugenzi mbadala asiye mtendaji wa Safaricom mnamo Agosti 2017. Till ni Afisa Mkuu Fedha wa Vodacom Group. Kabla ya hapo, alifanya kazi kama Mkurugenzi wa Fedha wa Vodacom South Africa kuanzia Februari 2014. Ana uzoefu wa zaidi ya miaka 15 ya kusaidia kuleta mabadiliko ya kifedha na kiuendeshaji kupitia utaalamu wake katika mikakati ya kifedha, uongozi wa masuala ya biashara, kuongeza mapato na faida katika mazingira ya kimataifa. Till amekuwa na utaalamu mkubwa na mafanikio katika mashirika makubwa ya kimataifa ikiwa ni pamoja na nafasi katika masuala ya fedha na biashara, ikijumisha Mkuu wa Fedha na Mkuu wa Njia za Uendeshaji wa Masoko na Mauzo huko Vodafone Romania. Alianza kazi na kushika nyadhifa mbalimbali kwenye kampuni ya T-Mobile iliyoko Ujerumani na vilevile akifanya kazi kama mshauri wa mikakati The Boston Consulting Group.

### Ali A Mufuruki, (60)

**Mkurugenzi huru**
**Mwenyekiti wa Vodacom Tanzania PLC**
*A Henry Crown Fellow of the Aspen Institute Shahada ya Sayansi katika Uhandisi*

Ali ni mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi ya Vodacom Tanzania. Aliteuliwa kama mkurugenzi huru asiye mtendaji wa Vodacom Tanzania mnamo Novemba 2017. Pia ni mwanzilishi, Mwenyekiti na Afisa Mtendaji Mkuu wa Infotech Investment Group Ltd, biashara ya familia yenye maslahi katika TEHAMA, vyombo vya habari, simu, hisa binafsi, biashara za rejareja na mali zisizohamishika katika nchi mbalimbali za Afrika na nje ya Afrika. Ni mjasiriamali Mtanzania, mhisani, msemaji wa umma na mtoa mafunzo ya uongozi. Ali pia ni mwanzilishi mwenza wa the Africa Leadership Initiative (ALI) ambayo lengo ni kutumia nguvu na vipaji vya viongozi wanaoibukia ndani ya Afrika ili kuimarisha uwezo wao wa kujenga jamii bora kwa ajili ya mataifa yao. Ni mwanzilishi mwenza na Mwenyekiti wa CEO Roundtable of Tanzania, jukwaa la majadiliano ya sera ambalo huwakutanisha Maafisa Watendaji Wakuu zaidi ya 150 wa kampuni zinazoongoza nchini Tanzania. Mnamo Desemba 2016, alitajwa na Rockefeller Foundation kama Bellagio Policy Fellow Resident kwa mwaka 2017. Kabla ya hapo, Ali alikuwa Mwenyekiti wa Shirika la Ndege la Taifa "ATCL" na vilevile Mkurugenzi na Mwenyekiti wa kwanza wa Kamati ya Ukaguzi wa Benki Kuu ya Tanzania. Hivi sasa ni Mwenyekiti wa Bodi za Msingi East Africa LTD (Kenya), Legacy Capital Partners Ltd (Tanzania); Trademark East Africa (Kenya), Chai Bora Ltd (Tanzania), AMSCO (Netherlands) na the National Environment Trust Fund of Tanzania (NETF). Pia ni mjumbe wa Halmashauri ya Chuo Kikuu cha Muhimbili cha Afya na Sayansi za Tiba (MUHAS) Dar es Salaam.

**Margaret Ikongo (62)**
**Mkurugenzi huru**
**Mwenyekiti Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji**
*Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara na masuala ya Fedha, Chuo Kikuu Huria Tanzania.*
*Cheti cha Kimataifa cha Usimamizi wa Viashiria Hatarishi, Taasisi ya Usimamizi wa ViashiriaHatarishi, Uingereza.*
*Mjumbe katika Taasisi ya masuala ya Bima, Uingereza.*

Margaret aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Pia ni mjumbe wa bodi ya wakurugenzi ya NMB Bank PLC na AAR Insurance Tanzania. Kabla ya hapo, Margaret alikaa kwenye Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF). Margaret ana uzoefu mkubwa katika masuala ya fedha na utawala bora akiwa ameupata kutokana na kufanya kazi katika tasnia ya bima ambapo alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima la Taifa kwa kupindi cha miaka kumi. Margaret pia alikuwa mshauri wa Kamishna wa Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania pamoja na Kaimu Mkuu wa Kurugenzi ya Ufundi.

## 4 Uteuzi wa wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji

Kupitia maazimio tofauti na kwa mujibu wa ibara ya 32(f) ya Katiba ya Kampuni, Ndg. Margaret Ikongo, Ndg. Thembeka Semane na Ndg. Winifred Ouko wakiwa wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji wachaguliwe kuendelea kuwa wajumbe wa kamati tajwa.

### Azimio la kawaida namba 9

"ILIAMULIWA KUWA Ndg. Margaret Ikongo achaguliwe kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji."

### Azimio la kawaida namba10

"ILIAMULIWA KUWA Ndg. Thembeka Semane achaguliwe kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji."

### Azimio la kawaida namba 11

"ILIAMULIWA KUWA Ndg. Winifred Ouko achaguliwe kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji."

Wasifu wa Ndg. Margaret Ikongo, Ndg. Winifred Ouko na Ndg. Thembeka Semane umeonyeshwa hapo chini.

**Margaret Ikongo (62)**
**Mkurugenzi huru**
**Mwenyekiti Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anatambuliwa kuwa mtaalamu wa fedha kwa madhumuni ya kamati hii**
*Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara na masuala ya Fedha, Chuo Kikuu Huria Tanzania.*
*Cheti cha Kimataifa cha Usimamizi wa Viashiria Hatarishi, Taasisi ya Usimamizi wa ViashiriaHatarishi, Uingereza.*
*Mjumbe katika Taasisi ya masuala ya Bima, Uingereza.*

Margaret aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Pia ni mjumbe wa bodi ya wakurugenzi ya NMB Bank PLC na AAR Insurance Tanzania. Kabla ya hapo, Margaret alikaa kwenye Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF). Margaret ana uzoefu mkubwa katika masuala ya fedha na utawala bora akiwa ameupata kutokana na kufanya kazi katika tasnia ya bima ambapo alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima la Taifa kwa kupindi cha miaka kumi. Margaret pia alikuwa mshauri wa Kamishna wa Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania pamoja na Kaimu Mkuu wa Kurugenzi ya Ufundi.

**Winifred Ouko (49)**
**Mkurugenzi huru**
**Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira na Uteuzi**
**Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anachukuliwa kuwa mtaalamu wa fedha katika kamati hii**
*Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Cornell, United States of America.*
*Mwanachama wa Taasisi ya Taaluma ya Uhasibu, Kenya.*

Winnie aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Winnie ana uzoefu mkubwa katika masuala fedha katika makampuni na miradi. Winnie ni Mkurugenzi Mtendaji wa Lattice Consulting, akiwa na uzoefu wa zaidi ya miaka 20 wa kutoa huduma za ushauri katika masuala ya fedha, pamoja na mikakati na mafunzo kwa wateja ndani ya Afrika na Amerika Kaskazini. Winnie ni mkurugenzi asiye mtendaji na mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi na Dharura ya Barclays Bank, Kenya. Pia ni mjumbe wa bodi ya Kenya Pooled Water Fund na mdhamini wa World Wide Fund Fr Nature (Switzerland), ambapo pia ni mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi.

**Thembeka Semane (43)**
**Mkurugenzi huru**
**Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anachukuliwa kuwa mtaalamu wa fedha kwa madhumuni ya kamati hii**
*Stashahada ya Juu katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Biashara cha Pretoria Gordon, Afrika Kusini Mwanachama wa Taasisi ya Taaluma ya Benki ya Afrika Kusini.*

Thembeka aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Thembeka ana uzoefu katika masuala ya biashara ukihusisha mikakati ya mashirika, utekelezaji wa mifumo ya biashara, miradi yenye thamani kubwa, utekelezaji na ufuatiliaji, utawala bora na vilevile usimamizi wa fedha. Thembeka ni mkurugenzi wa Linea Consulting (Pty) Ltd, mjumbe wa Kamati ya Udhibiti ya ACASA & ATNS, akiripoti kwa Waziri wa Usafirishaji wa Afrika Kusini na pia ni mjumbe wa Baraza la ICASA. Thembeka anafanya kazi kama mjumbe wa bodi wa Idara ya Makazi EAAB, Mwenyekiti wa Kamati yake ya Fedha na Uwekezaji na ni mjumbe wa Kamati za Ukaguzi na Dharura pamoja na ya Rasilimali Watu na Ujira. Pia ni mjumbe wa bodi na mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Dharura na Kamati ya Ujira ya Mbuga za Wanyama za Afrika Kusini. Vilevile, Thembeka ni mjumbe wa South African Heritage Resource Agency na Kamati ya Uthibiti na Usimamizi wa Utendaji wa Manispaa ya Sol Platje.

## 5 Uteuzi wa Ernst & Young kuwa wakaguzi huru wa Kampuni

Kuteua kampuni ya Ernst & Young Inc., kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji, kuwa wakaguzi huru wa Kampuni na kushikilia nafasi hiyo hadi mwisho wa mkutano mkuu ujao wa mwaka wa Kampuni.

### Azimio la kawaida namba 12

"ILIAMULIWA KUWA Ernst & Young Inc. wateuliwe kuwa wakaguzi huru wa Kampuni na kushikilia nafasi hiyo hadi mwisho wa mkutano mkuu ujao wa mwaka wa Kampuni."

Ufafanuzi: PricewaterhouseCoopers Inc., wamekuwa wakaguzi wa Kampuni kwa miaka mitano iliyopita. Kwa mujibu wa taratibu bora, Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji katika mwaka huu ilitangaza Ombi la Mapendekezo kuhusiana na huduma za ukaguzi huru. Kufuatia kumalizika kwa mchakato wa ombi la mapendekezo, Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji ikiungwa mkono na Bodi inapendekeza Ernst & Young Inc. wateuliwe kama wakaguzi wa Kampuni kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Machi 2020.

## 6 Gawio

Kuidhinisha gawio la Shi 24.31 kwa kila hisa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2019 kama ilivyopendekezwa na wakurugenzi. Gawio litalipwa kabla au Ijumaa ya tarehe 18 Octoba 2019 kwa wanahisa waliosajiliwa kwenye kitabu cha usajili baada ya kufunga biashara ya hisa tarehe 22 Agosti 2019.

### Azimio la kawaida namba 13

"ILIAMULIWA KUWA gawio la Shi 24.31 kwa kila hisa ya kawaida kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2019 limeidhinishwa."

## 7 Ada ya wakurugenzi

Kuidhinisha ada ya wakurugenzi wasio watendaji ya dola za Kimarekani 481 000 kuanzia tarehe 1 Agosti 2019 hadi hitimisho la mkutano mkuu ujao wa mwaka wa Kampuni, ili kuiwezesha Kampuni kuwavutia watu wenye uwezo, ujuzi na uzoefu unaotakiwa ili kutoa mchango unaofaa kwa Kampuni.

### Azimio la kawaida namba 14

"ILIAMULIWA KUWA kiwango cha ada ya mwaka ya wakurugenzi wasio watendaji cha dola za Kimarekani 481 000 kimeidhinishwa kwa mchanganuo ufuatao:

| | Pendekezo la ada US$[1] | Ada ya sasa US$ | % ya badiliko |
|---|---|---|---|
| Mwenyekiti wa Bodi | 150 000 | 150 000 | 0.0 |
| Mjumbe wa Bodi | 30 000 | 30 000 | 0.0 |
| Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | 15 000 | 15 000 | 0.0 |
| Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | 8 000 | 8 000 | 0.0 |
| Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira | 12 000 | 12 000 | 0.0 |
| Mjumbe wa Kamati ya Ujira | 4 000 | 6 000 | 0.0 |
| Mjumbe wa Kamati ya Uteuzi[2] | 3 000 | 0 | 0.0 |

1. Ada hii inajumuisha kodi zote ikijumuisha kodi ya zuio, inayolipwa kwa shilingi ya Kitanzania kwa wakurugenzi wazawa, randi ya Afrika Kusini kwa wakurugenzi wa Afrika Kusini na dola ya Marekani kwa wakurugenzi wengine. Ada hii inalipwa kila robo mwaka (kwa mikupuo minne) kwa mikutano ya kawaida isiyopungua minne kwa mwaka, mikutano maalum mitatu na Mkutano Mkuu wa Mwaka na wa dharura kama itahitajika.
2. Mwaka 2018, wajumbe watatu wa Kamati ya Uteuzi na Ajira walilipwa jumla ya US $ 18,000. Mwezi Machi 2019 kamati hii ilitengwanishwa na kuundwa kamati mbili – Kamati ya Ajira na Kamati ya Uteuzi ambapo wajumbe wawili wa Kamati ya Uteuzi watalipwa jumla ya US $ 6,000 na wajumbe 3 wa Kamati ya Ajira watalipwa jumla ya US$ 12,000. Kiuhalisia hakuna ongezeko la ada ya wakurugenzi.

## Tarehe ya kufunga rejesta

Tarehe ya kufungwa rejesta ya wanahisa wa Kampuni kwa madhumuni ya kustahili kuhudhuria, kushiriki na kupiga kura kwenye mkutano mkuu wa mwaka ni Alhamisi tarehe 22 Agosti 2019. Gharama zinazohusiana na kuhudhuria mkutano mkuu wa mwaka zitalipwa na wanahisa wenyewe.

Wanahisa wanaohudhuria mkutano mkuu wa mwaka watatakiwa kuonyesha hati ya hisa au risiti ya uwekezaji ya DSE na vitambulisho vinavyotambulika kama vile kitambulisho cha utaifa, kitambulisho cha kupiga kura, pasi ya kusafiria au leseni ya udereva. Usajili wa wanahisa au wawakilishi wao watakaohudhuria mkutano mkuu wa mwaka utaanza saa 1.30 asubuhi Ijumaa tarehe 20 Septemba 2019.

## Kushiriki kwa njia ya kielektroniki

Wanahisa au wawakilishi wao wanaweza kushiriki mkutano mkuu wa mwaka kwa njia ya kielektroniki. Mwanahisa (au mwakilishi wake) atahitaji kupiga simu +255 746 160 516 kabla ya saa 4:00 asubuhi Jumanne tarehe 17 Septemba 2019 ili Katibu wa Kampuni aweze kumpatia namba za kumwezesha kushiri kwa njia ya kielektroniki. Wanahisa wanaokusudia kushiriki kwa kutumia njia hii, wawasilishe kwa Katibu wa Kampuni fomu ya uwakilishi yenye maazimio, kabla ya saa 4:00 asubuhi Jumanne tarehe 17 Septemba 2019. Washiriki wapige simu dakika tano (5) kabla ya kuanza kwa mkutano mkuu wa mwaka.

## Mahudhurio na wawakilishi

Wanaostahili kuhudhuria, kuzungumza na kupiga kura kwenye mkutano mkuu wa mwaka ni wanahisa tu.

Wanahisa wanaweza kuteua wawakilishi kuhudhuria, kutoa maoni na kupiga kura kwa niaba yao. Mwakilishi si lazima awe mwanahisa wa Kampuni. Kwa wanahisa ambao ni makampuni, fomu ya uwakilishi inapaswa kujazwa na afisa aliyeidhinishwa na iwekwe muhuri wa Kampuni husika.

Upigaji kura utaendeshwa kulingana na Katiba na kanuni za Kampuni. Maazimio ya kawaida yatakayopitishwa katika mkutano mkuu huu yatapaswa kuungwa mkono na zaidi ya 50% ya kura za wanahisa. Azimio maalum litapaswa kuungwa mkono na angalau 75% ya kura za wanahisa.

Wanahisa wenye hisa zisizo kwa majina yao lazima wawapatie watunzaji au wawakilishi wao maelekezo ya kupiga kura katika mkutano mkuu wa mwaka. Kama mtunzaji au mwakilishi wako hatapokea maelekezo kutoka kwako, kama itakavyokuwa, itabidi kufanya maamuzi kulingana na mamlaka uliyoyatoa kwake.

Iwapo hukumshauri mtunzaji au mwakilishi wako, kulingana na makubaliano kati yako na mtunzaji au mwakilshi wako kwa muda wa mwisho uliotajwa ndani yake, kuwa utahudhuria mkutano mkuu wa mwaka au kutuma mwakilishi kukuwakilisha kwenye mkutano mkuu wa mwaka, mtunzaji au mwakilishi wako atajua kuwa hutahudhuria mkutano mkuu wa mwaka na hutatuma mwakilishi. Iwapo unataka kuhudhuria mkutano mkuu wa mwaka au kutuma mwakilishi, lazima umwombe mtunzaji wako kutoa barua inayohitajika kwako.

Fomu ya uwakilishi, inayopatikana kutoka kwenye tovuti ya Kampuni (www.vodacom.co.tz/investor-relations) pamoja na nakala ya hati ya hisa au risiti ya uwekezaji ya DSE ya mwanahisa, lazima iwasilishwe kwa Katibu wa Kampuni katika ghorofa ya 7, Vodacom Tower, Ursino Estate, Kiwanja namba 23, Barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam, Tanzania kabla ya saa 4:00 asubuhi Jumanne tarehe 17 Septemba 2019. Badala yake, fomu zilizotiwa saini kikamilifu pamoja na hati ya hisa au risiti ya uwekezaji ya DSE ya mwanahisa zinaweza kutumwa kwa baruapepe kwenda investorrelations@vodacom.co.tz na kuwasilisha fomu halisi ya mwakilishi siku ya mkutano.

Uwasilishaji wa fomu ya mwakilishi haumzuii mwanahisa kuhudhuria mkutano mkuu wa mwaka.

Imeidhinishwa na Bodi



Caroline M. Mduma
**Katibu wa Kampuni**
30 Agosti 2019

# Fomu ya Mwakilishi

**Vodacom Tanzania Public Limited Company**
(Imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
(Namba ya usajili 38501)
(ISIN: TZ1996102715 Ticker code: VODA)
('Vodacom Tanzania' au 'Kampuni')

| **Sehemu A**<br>**Ijazwe na wanahisa wote** | |
|---|---|
| **Jina Kamili** | |
| **Namba ya Akaunti ya CDS** | |
| **Idadi ya hisa zilizo katika Kampuni** | |

**Sehemu B**
**Wanahisa tu ambao wanataka kuteua watu wengine tofauti na Mwenyekiti kama mwakilishi wanapaswa kujaza sehemu hii**

Mimi (Sisi), m/watajwa katika Sehemu A hapo juu, m/wenye Akaunti ya CDS Namba na Idadi ya hisa zinazomilikiwa na Kampuni zilizoonyeshwa hatika Sehemu A hapo juu, tu/ninawateua (tazama maelezo 1 & 2)

| | |
|---|---|
| | au kumkwamisha, |
| | au kumkwamisha, |

**Mwenyekiti** wa mkutano mkuu wa mwaka kama mwakilishi wangu (wetu) kuhudhuria na kuzungumza na kupiga kura kwa niaba yangu (yetu) katika mkutano mkuu wa mwaka ambao utafanyika katika Ukumbi wa Mlimani City siku ya Ijumaa tarehe 20 Septemba 2019 kwa madhumuni ya kuzingatia na, ikionekana inafaa, kupitisha maazimio ya kawaida na maalum yatakayopendekezwa na katika kila kuahirishwa kwa mkutano na kupiga kura za kukubali au kupinga mkutano maazimio ya kawaida na maalum au kuacha kupiga kura kulingana na hisa katika mtaji uliotolewa wa Kampuni iliyosajiliwa kwa jina langu.

**Sehemu ya C**
**Ijjazwe na wanahisa wote**

Tafadhali wekala alama "x" katika nafasi husika, unataka kupiga vipi kura.
Ikiwa haijaelekezwa vingine, mwakilishi aliyetajwa katika Sehemu B hapo juu atapiga kura kama anavyofikiri inafaa.

| | | Ndiyo | Kupinga | Kuacha |
|---|---|---|---|---|
| 1. | **Azimio la kawaida namba 1**<br>Kuthibitisha kumbukumbu za mkutano mkuu wa mwaka uliofanyika tarehe 1 Oktoba 2018 | | | |
| 2. | **Azimio la kawaida namba 2**<br>Kuthibitisha kumbukumbu za mkutano mkuu wa dharura uliofanyika tarehe 14 Novemba 2018 | | | |
| 3. | **Azimio la kawaida namba 3**<br>Kupitisha taarifa za pamoja za mwaka za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2019 | | | |
| 4. | **Azimio la kawaida namba 4**<br>Kumchagua Hisham Hendi kuwa mkurugenzi | | | |
| 5. | **Azimio la kawaida namba 5**<br>Kumchagua tena Henry JC Surtees kuwa mkurugenzi | | | |
| 6. | **Azimio la kawaida namba 6**<br>Kumchagua tena Till Streichert kuwa mkurugenzi | | | |
| 7. | **Azimio la kawaida namba 7**<br>Kumchagua tena Ali A Mufuruki kuwa mkurugenzi | | | |
| 8. | **Azimio la kawaida namba 8**<br>Kumchagua tena Margaret Ikongo kuwa mkurugenzi | | | |
| 9. | **Azimio la kawaida namba 9**<br>Kumchagua tena Margaret Ikongo kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | | | |
| 10. | **Azimio la kawaida namba 10**<br>Kumchagua tena Thembeka Semane kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | | | |
| 11. | **Azimio la kawaida namba 11**<br>Kumchagua tena Winifred Ouko kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | | | |
| 12. | **Azimio la kawaida namba 12**<br>Kuchagua Ernst & Young Inc. kuwa wakaguzi wa Kampuni kwa mwaka unaoishia Machi 2020 | | | |
| 13. | **Azimio la kawaida namba 13**<br>Kuidhinisha gawio la Shi 24.31 kwa kila hisa | | | |
| 14. | **Azimio la kawaida namba 14**<br>Kuidhinisha ada ya mwaka ya wakurugenzi wasio watendaji cha dola za Kimarekani 481 000 | | | |

Imetiwa saini leo tarehe mwezi 2019

Saini: Saini:

**Fomu za wawakilishi zilizojazwa lazima zikabidhiwe ofisini kwa Katibu wa Kampuni ya Vodacom Tanzania PLC si zaidi ya saa 4:00 asubuhi siku ya Jumanne tarehe 17 Septemba 2019.**

# Maelezo ya fomu ya mwakilishi

1. Mjumbe anastahili kuhudhuria na kupiga kura katika mkutano mkuu wa mwaka anaweza kumteua mwakilishi mmoja au zaidi kuhudhuria, kupiga kura na kuzungumza kwa niaba yake katika mkutano mkuu wa mwaka. Mwakilishi anatakiwa asiwe mjumbe wa Kampuni. Iwapo mjumbe ni kampuni, fomu ya mwakilishi lazima ijazwe na kugongwa mhuri au kwa kuandikwa na afisa au wakili aliyeidhinishwa kwa maandishi.

2. Tafadhali weka alama 'X' katika nafasi husika kulingana na namna unavyotaka kura yako ipigwe. Hata hivyo, iwapo unataka kupiga kura yako kwa idadi ndogo zaidi ya hisa kuliko unazomiliki katika Kampuni ingiza idadi ya hisa ulizo nazo unazotaka kutumia kupiga kura. Ukishindwa kufuata hayo hapo juu itachukuliwa kuwa umemuidhinisha mwakilishi kupiga kura au kuacha kupiga kura katika mkutano mkuu wa mwaka kama anavyochukulia inafaa kuhusiana na kura zote za mwanahisa zinazotumika katika mkutano. Mwanahisa au mwakilishi wake hawajibiki kutumia kura zake zote zinazotumiwa na mwanahisa au mwakilishi wake, lakini jumla ya kura zilizopigwa na kuhusiana na zile za kuacha kupiga kura zilizorekodiwa hazitazidi jumla ya kura zinazotumiwa na mwanahisa au mwakilishi wake.

3. Mwanahisa anaweza kuingiza jina la mwakilishi wake au majina ya wawakilishi wawili mbadala wa chaguo la mwanahisa katika nafasi iliyotolewa, kwa kufufa au bila kufuta "Mwenyekiti wa mkutano mkuu wa mwaka" lakini ufutaji huo lazima utiwe saini na mwanahisa. Mtu ambaye jina lake ni la kwanza kwenye fomu ya mwakilishi na ambaye yupo katika mkutano mkuu wa mwaka atakuwa na haki ya kufanya kazi kama mwakilishi ukiondoa wale ambao majina yao yanafuata.

4. Fomu za wawakilishi pamoja na nakala ya risiti ya hisa za mwanahisa, lazima ziwasilishwe kwa ajili ya taarifa kwa Katibu wa Kampuni katika ghorofa ya 7, Vodacom Tower, Ursino Estate, Kiwanja Namba 23, Barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam, Tanzania kabla ya saa 4:00Asubuhi Jumanne tareha 17 Septemba 2019. Badala yake, fomu zilizosainiwa za wawakilishi na nakala ya hati ya hisa au risiti ya uwekezaji ya DSE za mwanahisa zinaweza kuskaniwa na kutumwa kwa baruapepe kwenda investorrelations@vodacom.co.tz. Mwakilishi anapaswa kuwasilisha fomu ya mwakilishi siku ya mkutano.

5. Ujazaji na uwasilishaji wa fomu hii ya mwakilishi hautamzuia mwanahisa husika kuhudhuria mkutano mkuu wa mwaka na kupiga kura yeye mwenyewe katika mkutano ukiondoa mwakilishi yeyote aliyeteuliwa kwa fomu hii ya mwakilishi.

6. Mabadiliko au marekebisho yoyote yaliyofanywa katika fomu hii ya mwakilishi lazima yatiwe saini na mtia/watia saini.

7. Mtu aliye na umri mdogo lazima asaidiwe na mzazi au mlezi wake isipokuwa kama nyaraka husika zinazobainisha uwezo wake kisheria ziwe zimetolewa.

8. Mwenyekiti wa mkutano mkuu wa mwaka anaweza kukubali fomu yoyote ya mwakilishi ambayo imejazwa vinginevyo tofauti kulingana na maelezo haya iwapo ameridhika na namna mwanahisa anavyotaka kupiga kura.

9. Where there are joint holders of shares:

Mmiliki yeyote mmoja anaweza kusaini fomu hii ya mwakilishi; na

Kura ya mwanahisa mwandamizi (kwa madhumuni hayo, uandamizi unaamuliwa na mpangilio ambapo majina ya wanahisa yanaonekana katika rejista ya kampuni) ambaye anapiga kura (iwe yeye mwenyewe au mwakilishi) itakubaliwa ukiondoa kura za wanahisa wengine wenza.




Ms Caroline Mduma
**Katibu wa Kampuni**
7th Floor, Vodacom Tower, Ursino Estate,
Plot 23, Bagamoyo Road,
PO Box 2369
Dar es Salaam
E-mail: investorrelations@vodacom.co.tz

# Taarifa kuhusu umiliki

| Jumla ya hisa | Machi 2019<br># ya hisa | % ya hisa[2] |
|---|---|---|
| Vodacom Group Limited | **1 092 000 130** | 48.7 |
| Mirambo Limited | **588 000 070** | 26.2 |
| Mfuko wa Pensheni wa Wafanyakazi wa Serikali (Uwekezaji wa Shirika la Umma SOC Limited, Jamhuri ya Afrika Kusini) | **164 503 540** | 7.3 |
| Wawekezaji wa Kitaasisi (Afrika Mashariki) | **244 835 925** | 10.9 |
| Wawekezaji wa Kitaasisi (Sehemu nyingine za dunia) | **45 830 302** | 2.0 |
| Wawekezaji wa rejareja | **95 833 853** | 4.3 |
| Wengineo[1] | **8 996 480** | 0.4 |
| | **2 240 000 300** | 100.0 |

**Note:**
1. Jumla ya hisa zinazomilikiwa, ikiwa ni pamoja na hisa zilizo chini ya kiwango cha uchanganuzi. Inaweza kujumuisha umiliki wa hisa za ziada za kitaasisi/rejareja.
2. Hakuna mabadiliko makubwa mwaka hadi mwaka katika mchanganuo wa umiliki kama ilivyoonyeshwa hapo juu.



## Umiliki wa hisa kitaasisi

| | Machi 2019, Umiliki kitaasisi kwa % |
|---|---|
| Tanzania | **47.9** |
| PIC | **36.1** |
| Afrika Kusini (Ukitoa PIC) | **8.3** |
| Uganda | **5.9** |
| United States | **1.8** |
| | **100.0** |

# Taarifa za Kampuni

## Vodacom Tanzania Public Limited Company
(imeandikishwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
Usajili namba: 38501
(ISIN: TZ1996102715 Share Code: VODA)

## Wakurugenzi
AA Mufuruki[1] (Mwenyekiti), H Hendi (Mkurugenzi Mtendaji)[8], JJ Marais (Mkurugenzi wa Fedha)[3], D Gutierrez[4], T Streichert[5], K Gomado[6], M Mbungela[3], ADJ Delport[3], M Ikongo[1], W Ouko[2], T Semane[3], HJC Surtees[7]

1. Mtanzania 2. Mkenya 3. Mwafrika Kusini 4. Mbolivia
5. Mjerumani 6. Mghana 7. Mwingereza 8. Mmisri

## Katibu wa Kampuni
Caroline Mduma

## Ofisi iliyosajiliwa
Ghorofa ya 15, Vodacom Tower,
Ursino estate, Kiwanja namba 23, Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P. 2369, Dar es Salaam, Tanzania

## Msajili Masuala ya Hisa
CSD & Registry Company Limited (CSDR)
Kambarage House,
Ghorofa ya 2 , Mtaa wa 6 Ufukoni
S.L.P. 70081, Dar es Salaam, Tanzania

## Mshauri Mkuu wa masuala ya Kumfadhili mjumbe mwenye leseni anayefanya biashara
Orbit Securities Company Limited

## Mawasiliano ya Nje
Rosalynn Mworia

## Mahusiano na Wawekezaji
Hilda Bujiku, Robin Kimambo
investorrelations@vodacom.co.tz
www.vodacom.co.tz/investor-relations